**Temeke** yatajwa kinara kesi za ukatili wa watoto

UKURASA 2



**Kilio** maiti, wagonjwa kubebwa kwenye machela

UKURASA 16


# Nipashe

Jumatatu Machi 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580513

MWANGA W… MII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**De Gea sasa awindwa PSG**

UKURASA 20

# Maziwa kutoka ng'ambo yakatazwa ofisi za serikali

• **Bodi** yaweka wazi sababu za marufuku hiyo...*Endelea Uk. 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MAWAZIRI WA BURUNDI, TANZANIA WATEMBELEA MIRADI YA KIMKAKATI**

MAWAZIRI watatu toka Tanzania na Burundi wametembelea miradi ya...

UKURASA WA 7

**2,162 HAWAJARIPOTI KIDATO CHA 1 LINDI**

WANAFUNZI 2,162 sawa na asilimia 13. kati ya 15,860 waliochaguliwa...


MAHOJIANO MAALUM

## Kesi ndoa, za mirathi zatikisa nchini

UKURASA 4



Rahel Nicolaus, mkazi wa Kijiji cha Kabita wilayani Busega mkoani Simiyu, ambaye pia ni mlengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), akielezea namna alivyobuni mbinu ya kujenga banda la mbuzi juu ya miti ili kuinusuru isiliwe na fisi, Habari Uk. 3. **PICHA: MARCO MADUHU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




# Mtawa auawa kikatili kwa kuchomwa kisu

UKURASA 2


**MICHEZO** **GOMES AFUNGUKA MORRISON KUACHWA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Temeke kinara ukatili wa watoto

**Na Devota Mwachang'a**

KESI za ulawiti na ubakaji zimetajwa kuwa kinara kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto katika Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam. Inaelezwa kuwa baadhi ya watoto hao wanalawitiana wenyewe kwenye vyoo vya shule wakati wa masomo.

Blandina Ndunguru, Mkaguzi msaidizi kutoka Dawati la Jinsia Kituo cha Polisi Chang'ombe Wilaya ya Temeke, akizungumza na Nipashe alisema takwimu za ulawiti miongoni mwa watoto wadogo zinazidi kupanda kadri miaka inavyozidi kwenda badala ya kushuka.

Alieleza kuwa walipokwenda kutoa elimu ya kukabiliana na ukatili kwa watoto shuleni wamegundua kuwa nusu ya wavulana darasa la kwanza na la pili ni waathirika wa ulawiti. "Uchunguzi wetu umebaini kuwa watoto wanalawitiwa na watoto wenzao wawapo shuleni, moja ya mbinu wanazotumia ni kuongozana wawili kwenda chooni... huko ndiko wanaitumia fursa wanakwenda kufanya ulawiti, pia hufanya kwenye nyumba (mapagala)," alisema Ndunguru.

Aidha, alisema matukio ya ukatili yanaendelea na mengi yanaishia mitaani hayafikishwi Dawati la Jinsia kwa hatua zaidi.

Alisema mbali na ulawiti kutekelezwa na watoto wenyewe kwa wenyewe wawapo katika mazingira ya shule, pia wapo wanofanyiwa ukatili huo na ndugu ndani ya familia zao. Kwa mujibu wa Ndunguru, wanapobaini tatizo na kuwahoji wahusika (watoto na wazazi wao) kutaka kujua watoto hao hufundishwa na nani, majibu huwa ni kutokana na kuangalia picha za ngono kwenye vibanda vya maonesho ya video mitaani.

"Sababu nyingine iliyobainika ni umasikini unaopelekea wazazi kulala chumba kimoja na watoto, hali hii hufanya watoto kushuhudia kwa siri pale wazazi wao wanapokuwa faragha wakiamini kuwa watoto wao wamelala fofofo," alibainisha.

Aidha, alikemea tabia ya baadhi ya wazazi kuruhusu ndugu wafikao nyumbani kulala pamoja na watoto wao. "Kuna ndugu huleta tabia zao mbaya kutoka kijijini, hivyo wasichanganywe na watoto pamoja, watoto walindwe wasilale na wageni wawe jinsia ya kike au kiume." Kwa mujibu wa Ndunguru, sheria bado haijakaa vizuri haitambui kumshtaki mtoto wa umri miaka 12 kwenda chini, hata hao wa kuanzia miaka 13 na kuendelea pia adhabu zao huwa ni ndogo kwa mujibu wa sheria.

"Wazazi wasikwame kwenye malezi, wasiwe wakali, wawe marafiki na wawafahamu watoto, waseme nao; mzazi akifahamu tabia za mwanae inamuwia rahisi kugundua kama mtoto amefanyiwa kitu cha tofauti kutokana na kuonekana mnyonge."

Katibu wa Kikundi cha Utetezi wa Haki za Wanawake na Watoto cha 'Tufashanwe' kilichopo Majohe-Ilala, Mariam Kivugo, bila kutaja takwimu, alithibitisha uwapo wa kesi nyingi za ubakaji dhidi ya watoto kwenye eneo lao ambazo humalizwa kiholela kwa makubaliano bila kufuata taratibu za kisheria.

Hivi karibuni katika hafla ya ufunguzi wa Kiwanda cha Ushoni na majengo ya Polisi Kurasini Manispaa ya Temeke, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro, akizungumza mbele ya Rais John Magufuli aliyekuwa mgeni rasmi, alisema Jeshi linakabiliwa na changamoto ya makosa ya jinai ikiwamo ubakaji kwa watoto.

# Marufuku maziwa ya nje ofisi za serikali

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Maziwa Tanzania, imesema ipo katika mpango wa kuelekeza kutotumika kwa maziwa wa unga kutoka nje ya nchi katika ofisi mbalimbali za serikali.

Aidha, imesema badala ya kutumia maziwa hayo yanayoagizwa kutoka nje, yatatumika yanayozalishwa na viwanda vya ndani.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Msajili wa maziwa nchini, Noely Byamungu, alisema wamebaini kwa sasa hakuna haja ya kuendelea kutumia maziwa kutoka nje ya nchi katika ofisi za umma kwa kuwa maziwa ya aina hiyo yanayozalishwa ndani ya nchi yanatosheleza mahitaji.

"Ni kweli tunapanga kuacha kutumia maziwa ya unga yanayoagizwa nje ya nchi kwenye ofisi za serikali kama ambavyo tumekuwa tukifanya. Serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa kuagiza maziwa ya unga nje ya nchi kwa ajili ya kuyasambaza kwenye ofisi za serikali," alibainisha Byamungu.

"Lakini kwa sasa tumeona hakuna haja hiyo kwa sababu viwanda vyetu vya ndani ya nchi vinatengeneza maziwa ya kutosha ya aina hiyo kwa sasa... mpaka sasa tuna viwanda vitano vinavyotengeneza maziwa ya aina hiyo na yanatosheleza mahitaji katika ofisi zetu mwaka mzima."

Kwa mujibu wa Byamungu, kuanza kutumia maziwa ya ndani katika ofisi za serikali, kutachangia pia kutangaza soko la maziwa ya ndani.

"Na ndiyo maana tukasema kama maziwa yanayotengenezwa nje ndiyo hayo yanayotengenezwa katika viwanda vyetu vya ndani, hakuna haja ya kuendelea kuyaagiza nje. Na tutakuwa tumeokoa gharama kubwa ambayo ilikuwa inatumika," alisema Byamungu.



Mkuu wa Kamandi ya Brigedi ya 202 Kundi la Vikosi, Brigedia Jenerali Julius Gambosi (aliyeshika fimbo), akimwongoza jana Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati (mwenye suti ya drafti), kuelekea eneo mojawapo la zoezi la utangulizi la kijeshi lililokuwa likijulikana kama Onesho Uwezo lililofanyika ndani ya Msitu wa Isawima kwa siku saba. **PICHA: VINCENT TIGANYA**

# Mtawa auawa kikatili kwa kuchomwa kisu

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MTAWA wa kituo cha kuhudumia wagonjwa wa ukoma cha Nazareth mjini Ifakara, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro, Agatha Mbalalila (50), ameuawa kwa kuchomwa kisu na mtu anayedaiwa kupokelewa katika kituo hicho kwa ajili ya matibabu.

Kifo cha mtawa huyo aliyekuwa muuguzi katika kituo hicho, kilitokea Machi 5, mwaka huu baada ya mmoja kati ya wagonjwa waliokuwa wakipatiwa matibabu katika kituo hicho (jina limehifadhiwa kwa upelelezi), kudaiwa kumchoma kisu wakati akielekea kuwahudumia wagonjwa wengine.

Akizungumzia kifo hicho, Katibu wa Kituo cha Nazareth, Ladislaus Mloti, alisema Agatha alimpokea mtuhumiwa huyo Februari 27, mwaka huu, baada ya kufika katika kituo na kujieleza kuwa ametoka katika matibabu ya ugonjwa wa ukoma Wilaya ya Bagamoyo.

Alisema baada ya kujieleza alionyesha kadi yake ambayo ilionyesha kuwa na matatizo ya ukoma na waliamua kumchukua na kumpima tena na kugundulika kuwa na tatizo hilo na kuanzishiwa matibabu mapya.

Alisema mtuhumiwa hakuwa na matatizo ya akili wakati anapokelewa na waliamua kumlaza ili kumpatia matibabu ya vidonda alivyokuwa navyo mguuni na wakaona busara waanze kumtibia vidonda hivyo na baada ya kupona wangemruhusu arudi nyumbani ili kuendelea na matibabu ya ugonjwa wa ukoma.

Siku ya tukio, Katibu alisema alifika kituoni baada ya kutoka kuchukua fedha, ikiwa ni maandalizi ya kuwanunulia nyama wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ifakara ambao walimuomba akawanunulie na wakati akijiandaa kuwasha gari alimuona Aghata akimkimbilia na kuomba amsaidie kumkimbiza hospitali ili kupatiwa matibabu.

Mloti ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mlabani, alisema wakati anakaribia kumsaidia Mtawa huyo alimuona mtuhumiwa kwa nyuma akimkimbiza huku akiwa na kisu mkononi na alipoona kundi la watu, aliamua kujichoma kisu tumboni na baadaye kuanguka chini baada ya kuishiwa nguvu.

Alisema alipoona Agatha anatokwa damu yeye na wafanyakazi wenzie waliamua kumkimbiza Hospitali ya Rufani ya Mt. Francis na baada ya kupokelewa alipewa taarifa muda mfupi baadaye kuwa mtawa huyo amefariki dunia.

Alisema kuwa walitoa taarifa Polisi na walipofika eneo la tukio walimkuta mtuhumiwa akiwa amejijeruhi tumboni huku utumbo ukiwa nje na kumchukua na kumpeleka hospitali.

Katibu huyo alisema, Agatha alikuwa muuguzi mkuu wa kituo hicho na alianza kazi miaka ya 90, licha ya kuwa muuguzi mkuu pia alikuwa mkuu wa nyumba ya masista wa kitengo cha Amani mjini Ifakara.

Mloti alisema shughuli za mazishi zinatarajiwa kufanyika kesho kwa mwili kuombewa katika kituo na Kanisa Kuu Katoliki la Ifakara na baadaye kusafirishwa kuelekea Itete wilayani Malinyi wanakozikwa watawa wa Shirika la Wafransisco.

Alisema tukio hilo ni la kwanza kutokea katika kituo hicho na kwamba hivi sasa wanajipanga kwaajili ya kuimarisha ulinzi kwa wagonjwa wanaoingia na waliopo.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mt. Francis Dk. Winfrid Gingo, alisema Agatha alifia hospitali wakati akipatiwa matibabu.

Alisema uchunguzi wa kifo chake umefanywa na daktari wa halmashauri ambaye bado hajawasilisha majibu, lakini Agatha alipofika hospitali alilalamika kuwa alichomwa kisu.

Kuhusu hali ya mtuhumiwa, alisema baada kupokelewa alifanyiwa upasuaji na kubainika mshipa mkuu wa kupeleka damu katika utumbo ulikatika baada ya kujichoma kisu cha tumbo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fotunatus Muslimu, akizungumza kwa njia simu, alisema hajapata taarifa rasmi juu ya tukio hilo na anawasiliana na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kilombero ili kupata taarifa zaidi.

## HABARI KITAIFA

# Abuni banda la mbuzi juu ya mti

**Na Marco Maduhu,** BUSEGA

RAHEL Nicolaus, mkazi wa kijiji cha Kabita wilayani Busega mkoani Simiyu, amejenga banda la mbuzi juu ya miti ili kuwaepusha mifugo hao kuliwa na wanyama aina ya fisi.

Nicolaus ambaye pia ni mlengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), alibainisha hayo mwishoni mwa wiki, wakati maofisa wa TASAF kutoka makao makuu walipotembelea walengwa wa mpango huo wilayani humo.

Alisema kutokana na fisi kuwa wengi kijijini humo, aliamua kukata miti na kisha kujenga banda la mbuzi juu ya miti hiyo, ili kuwaepusha kuliwa na wanyama hao, na kumrudisha kwenye umaskini.

"Katika kijiji hiki kuna fisi wengi sana, hivyo nikabuni mbinu ya kujenga banda la kuhifadhi mbuzi wangu juu ya miti, ili wawe salama na kwamba nina mpango wa kubadilisha na kuweka nguzo za chuma ili kuhakikisha usalama wao zaidi," alisema Nicolaus.

"Mbuzi hawa niliwapata kupitia fedha za ruzuku TASAF, na wamenisaidia sana kutatua shida zangu nyingi, ikiwamo kujenga nyumba hii ambayo mnaiona, na sasa nimebakiwa na mbuzi watano," aliongeza.

Ofisa ufuatiliaji wa TASAF wilayani Busega mkoani Simiyu, Gibanga Makoba, alisema kwenye kijiji hicho kuna tatizo la mifugo kuliwa na fisi, na kwamba kwa ubunifu wa mwanamke huyo ataweza kuwathibiti na kulinda mifugo yake.

Aidha, alisema asilimia 85 ya walengwa TASAF wilayani humo maisha yao ni mazuri, na kwamba wamejenga nyumba imara, wana mashamba, pamoja na mifugo, na wana walengwa 3,300 na tangu mwaka 2015 wameshatoa kiasi cha Sh. bilioni 4.9, kwa ajili ya kuzinusuru kaya maskini.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akiwa na baadhi ya wanawake aliowaongoza kufanya utalii wa ndani katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Mawaziri wa Burundi, Tanzania watembelea miradi ya kimkakati

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

MAWAZIRI watatu toka Tanzania na Burundi wametembelea miradi ya kimkakati inayoziunganisha nchi hizo mkoani Kigoma na kutoa maelekezo yanayoitaka miradi hiyo ikamilike kwa wakati ili kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mawaziri hao ni wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, Prof. Palamagamba Kabudi; Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Leonard Chamuriho na Waziri wa Mambo ya Nje wa Burundi, Albert Shingilo.

Akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Mnanila ambacho kipo katika mpaka wa Tanzania na Burundi wilayani Buhigwe mkoani Kigoma, Prof. Kabudi alisema Serikali imedhamiria kuufungua Mkoa wa Kigoma kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, reli, uwanja wa ndege wa Kigoma na bandari ili shughuli za usafirishaji ziweze kufanyika kikamilifu.

Aidha, alisema ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha mpakani utaimarisha utendaji wa maofisa wanaohusika na wananchi wanaotumia mpaka huo kuvuka na kupunguza kasi ya watu wanaotumia njia zisizo rasmi kuvuka na kuingia nchi nyingine.

Alisema miradi hiyo inafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, na kwamba miundombinu inayojengwa inaimarisha uhusiano ya kindugu kati ya wananchi wa Tanzania na Burundi pamoja na ulinzi na usalama katika eneo hilo.

"Pamoja na mtandao wa barabara, serikali za Tanzania na Burundi zinafanya jitihada za kuimarisha mawasiliano ya barabara na reli ili kurahisisha uchukuzi wa mizigo na watu kusafiri, lakini pia tunajenga reli-Uvinza -Kigoma hadi Msongati Burundi yenye urefu wa kilomita 240 ambapo kati kilomita hizo 84 zipo Burundi na matarajio ni reli hiyo kwenda mpanda Jamhuri ya kidemokrasi ya Congo," alisema Prof. Kabudi.

Naye Waziri Shingilo alisema hatua ya Burundi kuingia kwenye ukanda wa ushoroba wa kati itaisaidia nchi hiyo ambayo imewekewa vikwazo na Jumuia ya Kimataifa kukuza uchumi wake, na kwamba wananchi wa Burundi wako tayari kushirikiana na Tanzania katika kuinua na kukuza uhusiano wa kiuchumi na kijamii.

Kwa upande wake, Waziri Chamuriho akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Kasulu hadi katika mpaka wa Tanzania na Burundi, Mnanila yenye urefu wa kilomita 68 inayojengwa kwa kiwango cha lami, alisema haridhishwi na kasi ya ujenzi, na kuwataka wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha barabara hiyo inakamilika katika muda uliopangwa wa miezi 36.

Alisema zaidi ya Sh. bilioni 76.1 zinatumika kujenga barabara hiyo ikiwa ni sehemu ya ujenzi wa barabara inayounganisha mikoa ya Kigoma na Kagera yenye urefu wa kilomita 260.

"Ujenzi huu ni mkubwa, nawaomba wananchi mtoe ushirikiano wa dhati kwa makandarasi na viongozi ili kazi iende vizuri lakini pia muwe tayari kufanya kazi za ujenzi kwenye miradi hii," alisema.

# Waziri aagiza wanaozunguka migodi kupewa ajira kwanza

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imeiagiza kampuni ya Barrick Buzwagi na Bulyanhulu, kutangaza matangazo yote ya ajira kwenye mbao za matangazo katika maeneo yanayozunguka migodi hiyo. Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, alitoa agizo hilo jana katika ziara yake ya siku moja kwenye migodi hiyo eneo la uwekezaji lililotengwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama lenye hekari 2,100.

Alisema kuwa viongozi wa migodi hiyo wana wajibu wa kutoa matangazo ya ajira kwa wananchi wanaozunguka migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi ili wananchi waombe kazi na kuondoa malalamiko ya migodi kuwapa ajira watu kutoka nchi za nje na mikoa jirani.

"Tuna vijana wengi mitaani wanaozunguka migodi hii hawana ajira licha ya kuwa na ujuzi mbalimbali, wanashindwa kuona ajira kwa kutoona matangazo ya ajira, hivyo naagiza matangazo yote ya ajira yabandikwe kwenye mbao za mtangazo vijijini na ofisa za watendaji wa kata," alisema Katambi.

Mbunge wa Msalala, Idd Kasimu, alisema kuna ukiritimba katika masuala ya ajira zinazotolewa na migodi kwenda kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo suala ambalo linasababisha uhusiano kuwa mabaya baina yao na wananchi.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja Mkuu wa mgodi wa Bulyanhulu, Zumbi Musiba, alisema suala hilo amelipokea na atalifanyia kazi ili kuondoa malalamiko na kuwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi.

Mkazi wa kijiji cha Kakola, Kata ya Mulyanhulu, Erasto Venace, alisema mgodi unatoa ajira kwa mafundi ujenzi kutoka nchini za nje, wilayani na mikoa jirani, lakini wanaozunguka mgodi huo wanakosa ajira licha ya kuwa na ujuzi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA DODOMA MJINI

KITUO CHA CHAMWINO MJINI MKOA WA DODOMA

USIMAMIZI WA MIRATHI NA 12 2021

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MUSAMRI TINGWA KINDO WA MKUHUNGU
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MAUDUDI MUSAMRI TINGWA

**TANGAZO**

(kanuni ya 52 za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja katika shauri endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 mwezi MACHI mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 05 mwezi 03 mwaka 2021

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**LUCAS NICCO SINKALA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALLEX** yenye namba za usajili **T 669 DCP, Engine number-NZE120346721, chasis namba INZB67335**3. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa DAR/OST/RB/129085/2021

MAHOJIANO MAALUM

# Kesi za ndoa, mirathi zinavyotikisa nchini

## ■Tabora, Katavi balaa ndoa za utotoni
## ■Arusha yaongoza matukio ya ukeketaji

**Na Frank Monyo**

TANZANIA inaungana na nchi zingine duniani leo kuadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani. Siku hii hutumika kupima mafanikio ya utetezi na utoaji elimu kwa jamii katika safari za ukombozi wa mtoto wa kike juu ya madhira yote anayokutana nayo katika jamii.

Serikali, taasisi na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali yamekuwa mstari wa mbele katika kutetea kundi hilo, ili kuhakikisha kunakuwa na usawa katika jamii.

Nipashe imepata nafasi ya kufanya mahojiano na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala, kuhusu siku hiyo muhimu katika ukombozi wa mwanamke.

Lulu anasema ukatili wa kijinsia katika jamii hautaisha ikiwa jamii haitashiriki kutokomeza vitendo hivyo, ikiwamo kuachana na mila, desturi na fikra hasi dhidi ya mwanamke.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na ofisa huyo kuhusu mchango wa LSF katika ukombozi wa mwanamke na mambo mengine:-

**SWALI:** Mpaka sasa mmefanikiwa kuwafikia wananchi wangapi katika huduma zenu za msaada wa kisheria?

**LULU:** Tangu LSF ilipoanza kutekeleza mradi wa upatikanaji wa haki nchini takribani muongo mmoja sasa, imekuwa ikitoa ripoti kila mwaka kuonyesha ni jinsi gani mradi huu umekuwa na matunda katika jamii.

Kwa mujibu wa ripoti yetu ya mwaka 2020 juu ya utekelezaji wa mradi wetu nchini, takribani watu 99,844 wamepatiwa huduma ya msaada wa kisheria. Kati yao, wanaume ni 39,641 (asilimia 40) huku wanawake ni 60,203.

Pia, tumewafikia takribani watu milioni sita kwa kuwapatia elimu juu ya masuala mbalimbali ya sheria. Mafanikio haya yamekuwa chachu kubwa katika kuwezesha jamii kuwa na uelewa wa sheria na kujua haki zao na kisha kuzidi na kuzipata kwa maendeleo yao kwa ujumla.

**SWALI:** Kipi kikwazo kikuu katika utendaji na utekelezaji wa majukumu yenu ya kazi?

**LULU:** Tangu LSF ianze kufanya shughuli zake, kumekuwa na vikwazo kadhaa ikiwamo ukubwa wa nchi na miundombinu imesababisha huduma za msaada wa kisheria kutokufika kwenye kila kata.

Kwa sasa wasaidizi wa kisheria wanapatikana kila wilaya, lakini upande wa kata tumezifikia kata 1,750 kati ya kata zaidi ya 3,000. Tunaona iko haja kuongeza idadi ya watoa huduma za msaada wa kisheria na kuongeza ruzuku ili kufikia malengo haya.

Kikwazo cha pili ni cha muda mrefu wasaidizi wa kisheria walikuwa hawatambuliki kisheria na kufanya uwapo wao na utendaji wao kuwa na changamoto kubwa, lakini LSF kwa kushirikiana na wadau mbalimbali pamoja na serikali chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ilisaidia sana kuundwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017.

Sheria hii imewapa fursa wasaidizi wa kisheria kufanya kazi zao kwa uhuru kwa kuwa wanatambulika kihalali juu ya kazi zao wanazozifanya za kusaidia jamii huduma za msaada wa kisheria.

Kikwazo kingine ni kupungua kwa idadi ya wasaidizi wa kisheria waliopewa mafunzo kila mwaka. Hii inatokana na kwamba kazi hii ni ya kujitolea na hivyo tunaona iko haja kuweka mifumo bora ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, kuwapatia motisha na kuwawezesha wasaidizi wa kisheria kufanya kazi katika mazingira wezeshi zaidi.

**SWALI:** Ni kesi zipi mnazokutana nazo wakati wa kutoa msaada wa kisheria?

**LULU:** Kesi tunazokumbana nazo mara nyingi zinakuwa za madai pamoja na jinai. Katika mradi wetu, kupitia wasaidizi wetu wa kisheria, tunashughulika zaidi na kesi za madai ambazo zinakuwa bado hazijafika mahakamani.

Mara nyingi kesi ambazo zimeshafika mahakamani wasaidizi wetu wa kisheria huwa hawashughuliki nazo kwa kuwa ni nje ya maeneo yao ya kiutengaji.

Hata hivyo, kuna baadhi ya kesi zinazoshindikana mahakamani huwarudia wasaidizi wetu wa kisheria ambao hushughulika nao na wakati mwingine hufanikiwa kuzitatua kwa amani kabisa pasipo tatizo lolote.

Ikumbukwe kuwa kesi nyingi zinapelekwa mahakamani, lakini ni asilimia nne ndizo zinazomalizika. Hivyo, wasaidizi wetu wa kisheria bado wana kazi kubwa ya kufanya kuendelea kusaidia jamii.

**SWALI:** Ni matukio yapi mnayoyaona yamekithiri katika kesi mnazoshughulikia? Unadhani kwanini?

**LULU:** Kati ya kesi 99,844 zilizoripotiwa kwa mwaka 2020 kwa mfano, suala kubwa lilionekana kuripotiwa kwa kiwango kikubwa ni migogoro ya ardhi ambayo imeripotiwa kwa asilimia 33 ikifuatiwa na kesi za mirathi ambazo zimeripotiwa kwa asilimia 12, na migogoro ya ndoa ambayo nayo imeripotiwa kwa asilimia 11.

Katika migogoro ya ardhi 11,474 iliyoripotiwa na wanawake kwa wasaidizi wa kisheria ilitatuliwa huku migogoro mingine 1,749 ilipewa rufani ya kwenda kwenye vyombo vingine vya uamuzi wa kisheria kama vile mahakama na kesi 2,746 bado zinaendelea mpaka sasa.

Migogoro ya ardhi imeonekana kwa kiasi kikubwa kwa sababu ndiyo msingi wa uchumi wa watu hususani walioko katika maeneo ya vijijini. Watu walio wengi hutegemea shughuli za kilimo ili kuendesha maisha yao.

Ndiyo maana ardhi imeonekana kwa kiasi kikubwa kuwa sehemu ya kesi zilizoripotiwa zaidi na kimsingi migogoro ya ardhi ndiyo inaongoza zaidi.

**SWALI:** Mpaka sasa mmehudumia kesi ngapi za migogoro ya wanandoa na za wanawake kudai matunzo ya watoto?

**LULU:** Kama nilivyosema hapo awali, migogoro ya ndoa nayo imeripotiwa kwa kiasi kikubwa ukiachana na ya ardhi pamoja na mirathi.

Ripoti yetu inaonyesha kuwa kesi za migogoro ya ndoa 5,301 ziliripotiwa na wanawake, ambapo zilitatuliwa na kumalizika huku kesi 1,081 zikipatiwa rufani na kesi 1,134 bado zinaendelea mpaka sasa.

Kesi za migogoro ya matunzo ya watoto zilizoripotiwa na wanawake zilikuwa 5,949 ambazo zilitatuliwa na kumalizika kabisa huku kesi 1,062 zikipatiwa rufani kwa ajili ya hatua nyingine zaidi katika vyombo vingine vya sheria.

Kesi 1,013 za matunzo ya watoto bado zinaendelea kushughulikiwa mpaka sasa. Elimu bado inahitajika katika jamii ili kuhakikisha watu wanazitambua sheria.

Hii itasaidia watu kuepuka kufanya makosa ambayo yatawafanya waingie katika matatizo, mfano kutelekeza mtoto.

**SWALI:** Nini kifanyike kukomesha tatizo hili?

**LULU:** Vyombo vinavyosimamia sheria vinapaswa kuendelea kusimamia zaidi ili kuhakikisha kila mtu anakuwa chini ya sheria ili kujenga jamii yenye usawa pasi na kukandamiza mtu mwingine kwa sababu zozote zile.

**SWALI:** Tatizo la wanawake wajane kudhulumiwa mali ni kubwa kiasi gani katika jamii?

**LULU:** Kwa ujumla, wanawake ndiyo kundi kubwa linalokumbana na changamoto mbalimbali zinazohitaji huduma za msaada wa kisheria.

Kwa mujibu wa takwimu zetu, wanawake wanaongoza kwa kuripoti matukio mbalimbali yanayowakumba katika jamii kama vile kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi na ndoa, ukeketaji na hata mirathi.

Ripoti yetu ya mwaka 2020 inaonyesha kuwa kesi za mirathi takribani 11,555 ziliripotiwa, ambapo kesi 5,686 (asilimia 49) ziliripotiwa na wanawake.

Bado suala la mila potofu zinazochochea ukandamizaji wa mwanamke katika jamii. Ndiyo sababu ya kuendelea kuwapo kwa vitendo mbalimbali vya unyanyasaji wa kijinsia.

Mathalani, jamii ya wafugaji maeneo ya Arusha hasa Wilaya ya Ngorongoro kumekuwa utekelezaji wa mila mbovu zinazomkandamiza mwanamke na kumnyima haki ya kumiliki ardhi.

**SWALI:** Nini kifanyike ili kupunguza au kumaliza kabisa ukatili wa kijinsia nchini?

**LULU:** Kwanza, inapaswa kueleweka kuwa vita ya kupinga na kupambana na ukatili wa kijinsia ni ya kila mmoja wetu katika jamii pasipo kujali jinsia.

Hivyo, iwe mwanamke au mwanaume, kila mmoja wetu anapaswa kuwa mstari wa mbele katika kukemea vikali vitendo vya ukatili mbalimbali wa kijinsia.

Naamini kabisa, endapo kila mmoja wetu akiamua kuwa ukatili hauna nafasi katika jamii, basi vitendo kama hivyo vitamalizika.

Kila mmoja akiwajibika kwa nafasi yake tutatokomeza kabisa ukatili huu wa kijinsia.

**SWALI:** Maeneo gani ya nchi yamekithiri kwa matukio ya unyanyasaji wa wanawake na watoto?

**JIBU:** Mikoa ya Tabora na Katavi inatajwa zaidi kutokana na uwapo wa matukio mengi ya ndoa za utotoni.

Kuna mikoa ya Arusha na Manyara ambayo kwa pamoja inatajwa kuwa na vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia hususani ukeketaji. Asilimia 80 ya visa vingi vya ukeketaji viliripotiwa kutokea katika Mkoa wa Arusha.

Mila potofu katika jamii na uelewa mdogo juu ya athari ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile ukeketaji, ni sababu ya kuendelea kuwapo kwa matukio kama haya.

**SWALI:** Katika maadhimisho Siku ya Wanawake Dunia, mchango wa LSF ni upi katika jamii hususani wanawake?

**LULU:** LSF ni shirika lisilo la kiserikali linalowezesha upatikanaji wa haki hususani kwa wanawake. Tunawezesha upatikanaji wa haki kupitia watoa huduma za msaada wa kisheria, lakini pia tunawezesha jamii kujua sheria na kutambua haki zao kwani tunaamini mtu akijua sheria, ataitumia kudai haki yake na mwisho kuipata.

LSF tunatambua pamoja na kwamba masuala ya haki yanaikumba jamii nzima, lakini wanawake wanaathirika zaidi katika kupata haki zao za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kumekuwa na changamoto nyingi kwa wanawake kumiliki ardhi, kushiriki katika nafasi za uamuzi, kurithi mali na nyingine nyingi.

Programu hii ya upatikanaji wa haki inawajengea wanawake uwezo kwenye masuala ya kisheria, lakini pia tumewawezesha wale waliopata matatizo ya kupokonywa haki zao kuzipata. Katika kufanikisha haya yote, LSF inafadhiliwa na wadau wa maendeleo ambao ni DANIDA, DFID pamoja na Umoja wa Ulaya (EU).

**SWALI:** Corona imewaathiri vipi katika utendaji wenu?

**LULU:** Kuwapo kwa ugonjwa wa corona kumeathiri baadhi ya shughuli zetu zinazohusisha mkusanyiko wa watu wengi husani kazi zinazofanya na wasaidizi wa kisheria katika jamii za kutoa elimu kwenye mikutano na magulio.

Kazi hii zilisimama kabisa, lakini kumekuwa na ubunifu kama vile kutumia magari ya matangazo pamoja na kipaza sauti kutoa ujumbe, lakini ofisi za wasaidizi wa kisheria hazijafungwa bado wananchi wanaendelea kupatiwa huduma.

Covid-19 imetusaidia kufikiri njia mpya na za kibunifu kuweza kuwafikiwa wananchi kama vile kufanya mikutano yetu kupitia mitandao, kutumia redio, television na mitandao ya kijamii kufikiwa watu, kuanzisha 'mobile APP' itakayokuwa na uwezo wa kutoa mfunzo, kutoa msaada wa kisheria kwa jamii kupitia simu ya mkononi.

Tunachohofia sana ni pengine kupungua kwa ruzuku tunazopokea kutoka kwa wadau wa maendeleo. Hii inaweza kutokea kwa vile nchi nyingi za Ulaya zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na Covid-19.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala.


tigo pesa
Celebrating
10
years
Anniversary
Jana, Leo na Kesho
Tunaendelea kuwa Zaidi ya Pesa
tigo

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Namungo ibebeni vizuri Tanzania timu 4 CAF

**TAYARI** wawakilishi wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wamekamilisha mzunguko wa kwanza wa michuano hiyo hatua ya makundi wakiwa kileleni mwa msimamo wa Kundi A, linalozijumuisha Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan.

Simba ambayo ilianza kwa kushinda bao 1-0 ugenini dhidi ya AS Vita, kisha ikaibuka na ushindi kama huo ikiwa nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Al Ahly kabla ya Jumamosi iliyopita kulazimisha sare tasa nchini Sudan dhidi ya Al-Merrikh, imejikusanyia pointi saba hadi sasa mzunguko huu wa kwanza ukiwa umekamilika.

Kwa pointi hizo, ni wazi sasa Simba imejiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika, hasa kutokana na wapinzani wao wanaowafuata kwa karibu, AS Vita na Al Ahly kuwa na pointi nne kila moja huku Al-Merrikh ikiburuza mkia kwa alama moja.

Kwa sasa macho na masikio lakini pia na maombi kwa mashabiki wa soka nchini na Watanzania kwa ujumla, yameelekezwa kwa wawakilishi wengine wa nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo FC.

Miamba hiyo kutoka Ruangwa mkoano Lindi, ambayo ipo Kundi D pamoja na Pyramids ya Misri, Nkana FC ya Zambia na Raja Casablanca ya Morocco, keshokutwa Jumatano itaanza kibarua kigumu cha hatua ya makundi ikiwa ugenini dhidi ya Wamorocco hao.

Kwa ujumla tunatambua Namungo ipo kundi gumu hasa kutokana na ukweli kwamba timu itakazokutana nazo ni zoefu na kongwe kwenye michuano hiyo inayoshika nafasi ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Pamoja na ugumu huo, hatuna shaka na uwezo wa Namungo, kwani hadi kufika hatua hiyo, imeonyesha inaweza baada ya kuitoa timu kongwe na zoefu, CD de Agosto ya Angola kwenye mechi ya ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi.


Hivyo, tunaamini kama uongozi wa klabu, wachezaji na benchi la ufundi watakuwa wamejipanga vizuri kukabiliana na changamoto zote za nje na ndani ya uwanja, hakuna kinachoweza kuizuia Namungo kuandika historia mpya katika michuano hiyo.

Tunachotaka kwa sasa ni kuona Namungo nayo inabeba vema jukumu hilo la kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo kwa kujiweka katika nafasi ya juu kileleni mwa kundi lake ili kuondoa hofu ya kufuzu hatua ya robo fainali na kutimiza lengo la Watanzania kuona kwa mara ya kwanza Tanzania inafanikiwa kuingiza timu mbili hatua ya robo fainali kwa msimu moja.

Kadhalika, tunatambua kwa hatua tu ambayo Simba na Namungo zimefikia katika michuano hiyo ya CAF, tayari zimeiwezesha Tanzania kushika nafasi ya 12 kwenye viwango vya CAF kwa nchi zinazoruhusiwa kuingiza timu nne kwa msimu mmoja katika mashindano hayo, lakini bado inaweza kupoteza nafasi hiyo kama timu hizo hazitafuzu hatua ya robo fainali na nchi nyingine zinazoifukuzia zikifanya vizuri na kufika mbali zaidi katika michuano hiyo msimu huu.

Kwa mantiki hiyo, Watanzania kwa ujumla hatuna budi kuwa nyuma ya timu hizo kwa hamasa na maombi lakipi pia Simba na Namungo tukizitaka kutotazama mafanikio yao binafsi katika michuano hiyo, bali kutambua wajibu wao mkubwa katika kupigania nafasi ya Tanzania kuingiza timu nne msimu ujao na mingine mbeleni kwa kufika mbali zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuna haja sasa kwa Ligi ya Wanawake kuonyeshwa laivu

Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** si rahisi nchini kuona mashabiki wa soka wanahangaika kwa ajili ya kuangalia mechi ya soka la wanawake. Lakini katika hali isiyo ya kawaida, Ijumaa iliyopita mashabiki wa soka walijazana kwenye vibanda umiza, kwenye mabaa, mahotelini, kumbi mbalimbali za starehe, na hata kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kutazama mechi ya mahasimu wa jadi nchini, Simba Queens na Yanga Princess.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu ambayo Simba iliibuka na ushindi wa mabao 3-0, kilichovutia zaidi ni hamasa ile ile ya ushabiki wa klabu kubwa mbili nchini kama inavyokuwa kwa wanaume.

Ilikuwa si rahisi kuona mashabiki wa Simba wakifurahi eti timu ya wanawake imeshinda, au Yanga kuhuzunika kwa sababu timu yao ya kinadada imefungwa.

Lakini kwenye mechi hii hali ilikuwa tofauti. Mashabiki wa Simba walishangilia kama timu ya wanaume imeshinda na wa Yanga walionyesha kuhuzunika, pia kwenye vibanda umiza pamoja na kuangalia, lakini watu walikuwa wakibishana kuhusu mechi hiyo.

Wachezaji wa timu hizo nao hawakuwaangusha mashabiki, walicheza soka safi ambalo nadhani baadhi ya mashabiki walikuwa hawajawahi kuona kinadada wakicheza kwa kiwango cha juu kiasi hicho.

Uwezo mkubwa uliokuwa ukionyeshwa na kinadada hao uliwakuna wengine waliokuwa wanaangalia laivu kwenye televisheni na kusema kabisa kuwa hawakujua kuwa wanakosa uhondo kwenye Ligi Kuu ya Wanawake nchini Tanzania kwa kiasi hicho.

Mashabiki walipata burudani ya aina yake kutoka kwa wachezaji wa Yanga kwa kushuhudia kipaji kama cha kipa Husna Zuberi, Mrundi Aniela Uwimana, Neema Chibara, mpiga faulo wao matata, Happyness Mwaipaja, Fatuma Bushiri 'Tshishimbi' na straika wao hatari Aisha Masaka.

Kwa upande wa Simba ilikuwa ni starehe kuwaona Mwanahamisi Omari, kinara wa mabao kwenye ligi hiyo, Opa Clement, beki matata Juliet Singano, Asha Jaffar, Mrundi Joel Bukuru bila kumsahau dada wa Kikongomani Mawete Musolo aliyekuwa ndiye nyota wa mchezo kwa mashabiki wengi walioangalia mechi hiyo, kutokana na uwezo mkubwa aliouonyesha, akivaa namba 17, na vitu alivyokuwa akivifanya, mtaani tayari amepachikwa jina la Clautos Chama.

Hii ni mechi moja tu na tayari si tu mashabiki wameshaanza kuwafahamu wachezaji hao, lakini pia wanaonekana kutaka kufuatilia hata michezo mingine ya ligi inayoendelea.

Kutokana na hali hiyo, kuna haja sasa kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na wadhamini wa ligi wanaorusha matangazo kwenye luninga, kuanza kuonyesha baadhi ya mechi ili kuupa mchezo huo msukumo, nguvu na kuanza kupendwa na mashabiki kama ilivyo kwa upande wa wanaume.

Kumbe hakuna uchawi mwingine wowote wa kulikuza soka la wanawake, bali ni kuanza kuonyesha baadhi ya mechi na taratibu utaanza kuwa na mashabiki wengi ambao watakuwa wanafuatilia.

Kama ikiwa hivi, basi hata wadhamini wengine sasa wataanza kujitokeza na hiyo ndiyo njia ya kupata pesa ili kuboresha soka hilo na hata maisha ya kinadada hao, kwani posho zao zitaongezeka na kupata matunzo ya kambi nzuri, usafiri, chakula chao na maandalizi yatakuwa mazuri kuliko sasa.

Kuanza kuingia kwa baadhi ya watu kama Fatma Dewji kuwa mlezi wa Simba pamoja na Yvonne Cherry maarufu Monalisa kuteuliwa kuwa msemaji wa klabu hiyo, ni ishara nzuri kuwa soka la wanawake taratibu sasa linaanza kupanda juu.

Tunaona sasa kuna hata wachezaji wa kigeni kwenye soka la wanawake kama tulivyowashuhudia kina Uwinama, Bukuru na Mawete, hivyo sasa kinachohitajika ni ubunifu tu kwa TFF, hasa huu wa kuwaonyesha baadhi ya mechi.

Nasema hivi kwa sababu baadhi ya mashabiki walikuwa wanalalamika kuwa kumbe hata kwenye ligi ya wanawake kuna uhondo na wangetamani waendelee kuangalia, lakini huwa hawaonyeshi, hivyo inawapa tabu.

Niwapongeze TFF na Azam TV kwa kurusha mechi hiyo kwani imefanya wengi sasa kufahamu soka la wanawake lipoje au ligi yao iko vipi na wamekubali kama kiwango ni kile, basi ipo vizuri, kilichobaki tu sasa ni kufanya kama wanavyotaka.

Hii itafanya hata sasa watu waanze kulipa viingilio uwanjani kwa siku za usoni, kwani tayari watakuwa wameshapata uhondo na itakuwa ni faida kwa TFF, ligi yenyewe na timu zote za wanawake kwa ujumla, kwani bado zinatunzwa kwenye mazingira duni, lakini pia nchi itafaidika kwa mapato.

HABARI KITAIFA

# Shirika laiomba Serikali unafuu bei taulo za kike

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

SERIKALI imeombwa kusimamia upatikanaji wa taulo za kike kwa gharama nafuu ili kusaidia watoto wa kike kujihifadhi na kuhudhuria masomo yao vizuri.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwanasheria na Meneja Mipango wa Shirika la Wadada Solution Gender Based on Violence mkoani Mwanza, Anitha Samson, wakati akizungumza na Nipashe kuwa suala la taulo za kike ni tatizo kwa kuwa bei wanayouziwa ni kubwa ikilinganishwa na maisha ya baadhi ya wanawake.

Samson alisema hali hiyo huchangia wanafunzi wa kike kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi ili waweze kupata fedha za kununua na matokeo yake wanapata ujauzito na kusitisha masomo huku wakipoteza malengo yao.

"Serikali itambue umuhimu wa kupunguza bei ya taulo za kike najua, tamko likitoka serikalini kila mtu atafanya endapo litawekewa mkazo, maana mwanzo tamko lilitolewa na kodi iliondolewa kwenye bidhaa hizo, lakini mwisho wa siku bei ikabaki juu," alisema.

Alisema wengine wamelazimika kutumia kinyesi cha ng'ombe ambacho wanatengeneza kwa ajili ya kuweka kama taulo za kike huku wengine wakitumia vitambaa bila kuelewa namna ya kuvitumia.

"Unakuta mtu anaanika vitambaa sehemu ambazo hamna joto, havikauki vizuri na hawavipigi pasi ili kuua vidudu vinavyoweza kuhatarisha afya yao katika mfumo wa uzazi na pia kushindwa kuvifua vizuri kutokana na sehemu nyingine kuwa na tatizo la maji," alisema.

Alisema wanahamasisha watoto wa kiume kupigania watoto wa kike kupata elimu pamoja na kusisitiza utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kuanzia mtoto akiwa elimu ya msingi ili imsaidie katika ukuaji wake na kutimiza ndoto zake.

Kwa upande wake mmoja wa wakazi wa Kata ya Nyamanoro, Agnes Lucas, alisema ipo haja ya jamii, wadau na serikali kuchukulia suala la taulo za kike kama ajenda ya kudumu.

"Jambo hili tulichukulie kwa uzito wake maana nikitafakari watoto wanaoishi katika mazingira magumu kiukweli napata kigugumizi, inabidi lifanyike jambo hili taulo za kike zipatikane bure," alisema.

# 2,162 hawajaripoti kidato cha 1

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANAFUNZI 2,162 sawa na asilimia 13. kati ya 15,860 waliochaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari mkoani Lindi mwaka huu, hawajaripoti kwenye shule walizopangiwa kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo utoro.

Mshauri wa elimu katika Mkoa huo,Victor Kayombo, alibainisha hayo alipokuwa anazungumza na Nipashe, na kufafanua kuwa wanafunzi hao ambao hawajaripoti shule katika shule walizopangiwa hadi Februari 26, 2021,ni wasichana 1,157 na wavulana 1,005, huku Halmashauri za Nachingwea na Kilwa zikiongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto 533.

Kayombo alisema Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ina wanafunzi wasioripoti (481), Nachingwea (452), Mtama (390), Ruangwa (353), Liwale (292) na Lindi Manispaa (194).

Alisema kufuatia hali hiyo, baadhi ya wazazi na walezi wameanza kuchukuliwa hatua, ingawa hakuzitaja.




Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo, akiwa mbele ya pikipiki sita ambazo amewanunulia wasaidizi wake juzi, kwa ajili ya kurahisisha utendaji wa kazi zao za kumsaidia kuleta maendeleo jimboni humo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waliokuwa wafanyakazi Bulyanhulu wadai malipo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya watu 200 waliokuwa wafanyakazi wa mgodi wa Bulyanhulu, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, wamemuomba Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, kuingilia kati malipo ya stahiki zao.

Walitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki kwa Waziri Katambi kuwa tangu kusimamishwa kazi miaka 11 iliyopita mpaka sasa hawajalipwa stahiki zao. Mtumwa Mkweka, alisema alikuwa mfanyakazi wa mgodi wa Bulyanhulu tangu mwaka 1998 kama mlinzi na mwaka 2017 alisimamishwa kazi baada ya kuumia, lakini mpaka sasa hajalipwa stahiki zake. Alisema kuwa mgodi uliendelea kumhudumia kimatibabu na mwaka 2018 walisitisha matibabu na akarejea nyumbani na kwamba sasa anaonekana mzigo ndani ya familia yake.

Jamada Jabili, alisema alikuwa miongoni mwa wafanyakazi na aliumia kwenye uti wa mgongo akiwa kazini na mwaka 2015 aliondolewa kazini na kupewa Sh. 3,000,000, wengine Sh. 5,000,000 fedha ambazo hazikukidhi mahitaji kulingana na ugonjwa waliopata.

Alisema kuwa kwa sasa hawezi kufanyakazi yoyote.

Kwa upande wake, Katambi alikiri kutambua malalamiko hayo ambayo yalifika ofisini kwake na kwamba nyaraka zao zipo na kuwaomba kuwa na subira.

# Fedha za ng'ombe zilivyomponza kupata kilema

**Na Samson Chacha,** RORYA

MKAZI wa Kijiji cha Kitembe, Kata ya Kitembe tarafa ya Girango, wilayani Rorya, Peter Ochieng (53), amenusurika kifo baada ya kukatwa mapanga na watu wanaodaiwa kuwa ndugu zake waliokuwa wanataka fedha alizouza mifugo na kumsababishia kilema cha mikono.

Watuhumiwa hao wametajwa kuwa ni Omolo Oyugi na Kwaga Oyugi, waliokuwa na silaha za jadi ambao wanadaiwa kumvamia Ochieng nyumbani kwake usiku akiwa amelala na kuvunja mlango na kuanza kumkata kwa mapanga huku wakimtaka atoe fedha alizokuwa maeuza ng'ombe wake wawili.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Kijiji cha Kitembe wilayani Rorya, mwishoni mwa wiki, Ochieng alisema Januari 4, mwaka huu alipeleka ng'ombe wake wawili kuwauza katika mnada wa Randa wote kwa Sh. 1,200,000.

Alisema wakati akiuza mifugo yake ndugu zake walimuona akipokea fedha hizo.

Alisema ilipofika usiku saa nane alisikia mlango wa nyumba yake ukivunjwa na alipoamka na mke wake kupiga kelele za kuomba msaada kwa majirani, wahalifu hao, walianza kuwashambulia kwa kumkata mapanga kichwani, mgongoni, kifuani na mikononi na kumsababishia kilema.

Kamanda wa Polisi Tarime Rorya ACP William Mkonda, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kudai kuwa mtuhumiwa Omolo Oyugi, amekamatwa na Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka mtuhumiwa wa pili Kwaga Oyugi, ili kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

# Kunenge aagiza viongozi kutatua kero za wananchi

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, amewataka viongozi wa mkoa huo kutimiza majukumu kwa kutatua kero za wananchi na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha kwanza cha kamati ya ushauri ya mkoa (RCC) kilichofanyika Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Ummy Mwalimu.

Aliwataka viongozi kujadili na kushauriana kuhusu maendeleo ya mkoa na kuhakikisha wanajibu kero za wananchi kimkakati na kuboresha maisha yao. Alisema kila wanapofanya ziara kwa wananchi wanakutana na kero nyingi ikiwamo za taka na barabara ambazo kimkakati zinatakiwa kutatuliwa kwa mustakabali wa maendeleo ya wananchi na taifa.

Alisema viongozi wana wajibu wa kuhakikisha vipaumbele wanavyo viweka kwaajili ya wananchi vinakuwa sahihi na kusimamia yanayotakiwa kufanyika.

Aliwafahamisha wajumbe kuwa ofisi yake ilipokea magari 20 yatakayosaidia utunzaji wa mazingira kwa kukusanya taka.

Waziri Ummy wakati wa kuwasilisha muongozo wa mazingira katika usafishaji wa mito na kuondoa taka ngumu kwenye mkoa huo, alisema kumekuwa na uchimbaji holela wa mchanga ambao unasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira unaochangia kuharibika kingo za mito kupanuka.

Alisema alipata taarifa katika Wilaya ya Kinondoni ndani ya kipindi cha miaka mitatu nyumba 209 zilianguka sababu ikitajwa kuwa ni uchimbaji holela wa michanga kwenye mito na mabonde.



Wakili Rehema Mmanga akitoa elimu ya haki za wasichana na kupinga ukatilli wa kijinsia kwa wanafunzi wa Mugabe Sekondari, jijini Dar es Salaam juzi ambayo Chama cha Wanasheria cha Tanganyika kupitia Kamati ya Jinsia na HIV/AIDS ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo inafikia kilele chake kesho. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mpango wa bima kwa vikundi waanza

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi (NEEC), kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya Sanlam General pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) wamezindua mpango wa bima kwa vikundi vya VICOBA ili kuongeza ushiriki wa vikundi hivyo katika sekta za fedha na kupunguza gharama wanapofikwa na majanga au vifo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam baada ya uzinduzi wa mpango huo, Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'I Issa, alisema NEEC itafanya kazi ya kuratibu na kusimamia mpango huo pamoja na kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanatimia.

"Baraza limekuwa likiwaunganisha wananchi na fursa za kiuchumi hivyo ujio wa Sanlam utaongeza chachu ya wananchi kujua umuhimu wa Bima katika kuchochea maendeleo ya nchi lakini pia kukabiliana na changamoto ambazo wananchi wamekuwa wakikumbana nazo wakati wa majanga na vifo," alisema Beng'I. Aidha, alisema Baraza litatengeneza mwongozo wa usimamizi wa mpango huo, unatekelezwa ikiwa pamoja na kuwaunganisha waratibu wa uwezeshaji walioko kwenye mikoa/halmashauri na watendaji wa Sanlam ili wawafikie wananchi. Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam, Geofray Masige, mbali ya kuipongeza Serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya kushirikisha wadau wa sekta binafsi ili kutatua changamoto za wananchi, alisema makubaliano hayo ni hatua muhimu ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo hususani wanaofanya shughuli zao kwenye vikundi nchi nzima. "Gharama ya bima hii kwa kila mwana kikundi ni Sh.7,000 kwa mwaka na Sanlam itatoa mkono wa pole kwa mwanachama au mrithi atakapofariki kifo cha kawaida au cha ajali," alisema na kufafanua kuwa kwa kifo cha kawaida mwanachama atalipwa Sh.1,000,000 na kifo cha ajali ni Sh. 2,000,000 wakati vifo vya warithi wao Sanlam itatoa mkono wa pole wa Sh. 500,000.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Tafiti na Maendeleo ya Masoko kutoka TIRA, Zakaria Muyengi, alisema wao wataendelea kusimamia utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa bima.

## Gairo yapitisha bajeti zaidi ya bil. 20/-

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro, wamepitisha bajeti ya Sh. 20,985,913,464.72 katika mwaka wa fedha 2021/2022 zinazotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato wilayani hapo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Rachael Nyangas, kwenye kikao cha Baraza la Madiwani ambao wote waliomba bajeti hiyo itumike kuleta maendeleo ya wananchi kila kata.

"Nachukua fursa hii kuwashukuru madiwani wote kwa kuipitisha bajeti hii, ni matumaini yangu kuwa wilaya yetu ya Gairo itapata maendeleo makubwa katika maeneo mbalimbali hasa kwenye kata zetu sisi madiwani," alisema Rachael.

Alisema miongoni mwa miradi ambayo imeelekezwa katika bajeti hiyo ni pamoja na kuendeleza kilimo cha mazao ya kimkakati ikiwamo korosho, pamba, ufuta, kahawa na katani na pia kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kuongeza mapato.

Kwa upande wao madiwani waliomba fedha zote zitumike kuleta maendeleo yaliyokusudiwa ili kila mwananchi kwenye kata yake apate kunufaika kutokana na maendeleo mbalimbali yatakayokuwapo.

## Watakiwa kushirikiana kudhibiti uvuvi haramu

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

WANANCHI wametakiwa kushirikiana kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Victoria ili kuendelea kunufaika na rasilimali zake.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alitoa wito huo mwishoni mwa wiki katika kikao cha wadau wa uvuvi Kanda ya Ziwa, kuhusu ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

Mashimba alisema suala hilo ni jukumu la kila mmoja katika ngazi zote kuanzia kitongoji mpaka wilaya ili kuudhibiti.

"Ikiwa uvuvi haramu tutaukumbatia tutajiangamiza wenyewe, ninyi mnaofaidika na ziwa mpo na athari mnaiona kwanini waje maaskari kutoka Dodoma au sehemu nyingine kuja kufanya msako kwenu, ndugu zangu naomba tushirikiane wote, ngazi ya kitongoji, kijiji, kata wote hili ni jukumu letu suala la uvuvi haramu halikubaliki," alisema Ndaki.

"Ipo dhana inayozungumzwa kuwa uvuvi haramu ni dhana tu inayojengwa na wataalamu na serikali na kuna dhana nyingine kuwa samaki wapo tu ziwani na kuongeza kuwa ikiwa uvuvi haramu tutaukumbatia tutajiangamiza wenyewe," alisema.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi (BMU), Wilaya ya Rorya, Stephano Mchoye, alitaka halmashauri kushirikiana na vikundi hivyo ili kudhibiti uvuvi haramu kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

"Ulinzi shirikishi katika ziwa letu haujaanza leo, ninaomba wizara iangalie zana hizi zinazotumika katika uvuvi haramu zinatoka wapi dawa ya hiyo ikishapatikana naamini uvuvi haramu Tanzania hautapatikana," alisema Stephano.

HABARI KITAIFA

## Wanawake changamkieni fursa zabuni za umma-PPRA

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) imewahamasisha wanawake kuchangamkia fursa za zabuni za umma ili kujikomboa kiuchumi kwa kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma inawatambua na imewapa nafasi ya kipekee.

Katika ujumbe wake kwa umma, Mkurugenzi wa Kujenga Uwezo na Ushauri kutoka PPRA, Mhandisi Mary Swai, alisema kuwa katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, wanawake na jamii kwa ujumla inakumbushwa kuwa sheria imewatambua wanawake kama moja ya makundi maalum.

"Maboresho ya sheria yaliyofanyika yameweka makundi maalum ambayo ni wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu. Kutokana na umuhimu wa wanawake, sheria inawataka waingie kwenye zabuni zinazotangazwa na Serikali kwa sababu ni fursa," alisema Mhandisi Swai.

Aidha, alieleza kuwa hatua hiyo ya mabadiliko ya sheria imetokana na uhalisia kuwa ukimwezesha mwanamke kiuchumi utakuwa umeiinua jamii nzima kiuchumi kuanzia ngazi ya familia.

Alisema kwa kuzingatia hilo, mamlaka imekuwa ikitoa mafunzo bure kwa kwa wanawake ili kujengea uwezo wa jinsi ya kushiriki fursa za zabuni za umma. Ameongeza kuwa katika mafunzo hayo hushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), ambalo huwapa wanawake hao elimu kuhusu fursa za mifuko inayotoa mitaji kuwawezesha.

"Kwenye hayo mafunzo tunayofanya, NEEC inatoa mada inayowaeleza mifuko iliyopo ya kuwasaidia. Unakuta wengi hawajui kama kuna mifuko mingi ambayo wanaweza kuichangamkia ikaongeza mitaji yao na baadaye wakarudisha kidogo-kidogo. Kuna mifuko zaidi ya thelathini (30) ambayo Baraza linawaeleza. Kwahiyo, ni wao tu kuchangamkia fursa," alisema Mhandisi Swai.

Pia, aliwakumbusha wanawake kuwa Serikali imeweka utaratibu mzuri zaidi wa kumwezesha kila mwanamke. Kwamba katika kila Halmashauri kuna idara inayoshuhulika na wanawake, na katika kila makusanyo ya Halmashauri husika kuna asilimia zinazoenda kuwawezesha wanawake.

Amewataka wanawake wenye kipato cha kawaida au cha chini kuachana na fikra kuwa kushiriki tenda za Serikali kunahitaji kuwa na mitaji mikubwa, kwani zipo tenda ambazo zinahitaji mitaji midogo. "Sio lazima kuwa na mitaji mikubwa, tenda za Serikali zina mambo mengi, kuanzia madogo hadi makubwa. Mfano kuna tenda za kufanya usafi, tenda za migahawa ambazo Serikali inaweza kuhitaji hizo huduma na kuna tenda ndogondogo za bidhaa ndogondogo," alisema.

Mkurugenzi huyo wa PPRA amesema kuwa hivi sasa kuna mabadiliko makubwa kwenye sekta ya ununuzi wa umma kwenye upande wa usawa wa kijinsia, kwani wapo wahandisi wengi wanawake, na kwenye miradi mingi mikubwa hivi sasa kuna wanawake wanaosimamia vizuri miradi hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Abasi Kayanda, akipata maelezo kutoka kwa Angela Malley, mmoja wa wakulima kuhusu hatua waliofikia kwenye kampeni zao za kustawisha mbegu za asili za mazao mbalimbali yaliyothibitishwa na wataalam kuwa na virutubisho na pia kinga za magonjwa mbalimbali. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

## Wizara yataka taasisi zake kutumia vyombo vya sheria

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu), Andrew Massawe, ameziagiza taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kuvihusisha vyombo vya sheria katika kutekeleza majukumu yao ili kuleta usawa na uwajibikaji miongoni mwa taasisi husika na wadau wao.

Taasisi hizo ni pamoja na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Idara ya Kazi, Tume ya Uamuzi na Usuluhishi (CMA), Mfuko wa Hifadhi kwa Jamii wa Sekta Binafsi (NSSF), Mfuko wa Hifadhi kwa Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Maagizo ameyatoa jijini Dar es Salaam alipokuwa anafunga semina kuhusu Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi Na. 5 ya mwaka 2003 iliyotolewa na OSHA kwa Mawakili wa Serikali chini ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP).

Alisema taasisi hizo zinapaswa kushirikiana na vyombo hivyo vya dola kwa kutoa mafunzo kwa watumishi katika vyombo hivyo ili kuleta uelewa wa pamoja katika utekelezaji wa sheria mbalimbali ambazo utekelezaji wake unasimamiwa na taasisi hizo.

"Kuna kuwa na ugumu endapo kila taasisi itapambana peke yake katika kushughulikiwa masuala mbalimbali ya kisheria yanayoihusu hivyo ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sheria zenu ni muhimu sana kuvishirikisha vyombo vya kisheria vya serikali ikiwemo Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP), Wakili wa Serikali (Solicitor General), Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Attorney General) na Jeshi la Polisi," alisema Massawe

Akifungua semina hiyo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema lengo la semina hiyo ni kujenga uelewa wa pamoja baina ya OSHA na Mawakili wa Serikali ili kurahisisha utekelezaji wa sheria husika.

"Tunaamini kwamba kupitia mafunzo haya ya leo mtapata kufahamu kwa undani dhumuni kuu la Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 na pia namna ambavyo OSHA inasimamia utekelezaji wa sheria husika na hivyo tutaweza kushirikiana vizuri katika kuhakikisha kwamba sheria inatekelezwa ipasavyo," alisema Mwenda.

## 70 wafadhiliwa masomo ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imetangaza kutoa nafasi mpya 70 za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wanaosomea kilimo hapa nchini.

Ufadhili huu unajumuisha ada pamoja na gharama nyingine zote za masomo katika kipindi chote mwanafunzi anapokuwa chuoni.

Hii ni mara ya pili SBL inatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao na ambao wanatoka katika familia zenye vipato duni. Mwaka jana wakati SBL ikizindua mpango wake wa ufadhili wa masomo ya kilimo unaojulikana kama Kilimo Viwanda, ilitoa ufadhili kwa wanafunzi 40.

Programu ya Kilimo-Viwanda inalenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kuongeza idadi ya wataalamu wa kilimo hapa nchini, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti.

Akitangaza wanafunzi 15 waliopata ufadhili huo kwa mwaka huu kutoka Chuo cha Kaole Wazazi College of Agriculture cha Bagamoyo mkoani Pwani, Ocitti alisema pamoja na kutoa ufadhili wa masomo kampuni hiyo pia inafanya kazi na wakulima 400 ambao mwaka jana waliiuzia SBL tani 17,000 za nafaka sawa na asilimia 70 ya mahitaji yake ya malighafi kwa ajili ya kutengenezea bia.

"Uhusiano wa SBL na sekta ya kilimo una historia ndefu. Kwa sasa kampuni inafanya kazi na mtandao wa wakulima 400 kwenye mikoa nane hapa nchini ambapo tunanunua shayiri, mahindi na mtama kwa ajili ya uzalishaji wa bia zetu. SBL huwasaidia wakulima hawa kwa kuwapatia mbegu za bure, huduma za ughani pamoja na kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mikopo na kupanua uzalishaji wao," alisema. Mkuu wa chuo cha Kaole Wazazi College of Agriculture, Sinani Simba, aliishukuru SBL kwa kuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono maendeleo ya sekta ya kilimo ambayo ni sekta mama inayoajiri Watanzania wengi kuliko sekta yeyote ile. "Mafunzo kwa ajili ya wataalamu wa kilimo ni moja kati ya vipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Awamu ya Pili. Wataalamu wa kilimo ni muhimu katika kuwasaidia wakulima kuboresha shughuli zao kwa kuwaelekeza namna ya kulima kitaalamu ili kuongeza uzalishaji na kuboresha vipato vyao," alisema mkuu huyo wa chuo.

Kampuni ya SBL inashirikiana na vyuo vinne vya hapa nchini katika kutoa uhifadhili wa masomo chini ya Programu ya Kilimo Viwanda. Vyuo vingine ni Kilacha Agriculture Institute kilichopo Moshi mkoani Kilimanjaro, Igabiro Institute of Agriculture kilichopo Bukoba mkoani Kagera na St. Maria Goretti Agriculture Training Institute kilichopo mkoani Iringa.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper akizindua kampeni ya Promosheni ya NMB Bonge la Mpango kwa Kanda ya Mashariki mkoani Morogoro. Kushoto ni Meneja Mwandamizi Kilimo Biashara wa NMB, Isaac Masusu. Benki ya NMB jana kwa mikoa minne ( Mtwara, Morogoro, Kilimanjaro na Zanzibar), ilizindua kampeni ya bonge la mpango inalenga kutambua na kuthamini utamaduni chanya wa wateja kujiwekea akiba, ikiwa ni pamoja na kurejesha sehemu ya faida ya benki hiyo kwa mwaka uliopita, ambako NMB ilipata faida ya zaidi ya Sh. Bilioni 205. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 400/- zawajengea hosteli wanafunzi wa kike

**Na Stevie Chindiye,** SONGEA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma imetumia Sh. milioni 400 kujenga hosteli tano katika shule za sekondari ikiwa ni juhudi za serikali kuwapunguzia kero wanafunzi wa kike.

Hayo yamebainishwa na Ofisa Mipango wa Halimashauri hiyo, Athumani Nyange, na kueleza kuwa kila hosteli imegharimu Sh.milioni 80, na kwamba fedha zilizotumika kutekeleza mradi huo zilitolewa na Serikali kwa ajili ya kujenga hosteli katika shule za sekondari Matimira, Kilagano, Maposeni, Mpitimbi na Mhalule.

Nyange alisema Halmashauri ilipokea fedha hizo Agosti 2020, kwa ajili ya kutekeleza mradi huo ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 100, na kwamba kinachosubiriwa ni kuweka vitanda na hosteli kuanza kutumika.

"Kila hosteli ina nyunba 20 na ina uwezo wa kubeba wanafunzi 80 na kila chumba kinachukua wanafunzi wane, hivyo kwa niaba ya wananchi tunaishukuru sana serikali kwa sababu hosteli hizi ni ukombozi kwa watoto wa kike," alisema Nyange.

Mwalimu Selestin Mlelwa, Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mhalule, alisema mradi wa hosteli katika shule hiyo umekamilika na kusisitiza kuwa hosteli hiyo itakuwa ukombozi kwa watoto wa kike ambao wamekuwa wanatembea kilometa tisa kila siku kwenda na kurudi shuleni. Mkuu wa Shule ya Sekondari Mpitimbi, Patrick Matembo, aliishukuru serikali kwa kuipatia shule hiyo zaidi ya Sh. milioni 106 kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu ambayo ni hosteli moja iliyogharimu Sh. milioni 80, darasa moja Sh. milioni 20 na ujenzi wa choo matundu sita uliogharimu Sh.milioni sita.

Akiongea kwa niaba ya wanafunzi wa kidato cha sita sekondari ya Mpitimbi, Elizabeth Mwakyusa, aliishukuru serikali kwa kuwajengea hosteli, na kuwa hatua hiyo itawaongezea wanafunzi ari ya kusoma na kuongeza ufaulu.

# Maboresho Bandari Kigoma yapaisha mapato

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Deusidedit Kakoko, amesema maboresho makubwa yaliyofanywa katika Bandari ya Kigoma yameanza kuleta matokeo chanya ikiwamo kuongeza shehena ya mizigo pamoja na mapato.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Bandari ya Kigoma, Kakoko alisema shehena na mapato katika bandari hiyo yameizidi Bandari ya Mwanza ambayo awali ndiyo iliyokuwa ikiongoza kabla ya maboresho katika bandari hiyo ya Kigoma.

Alisema Bandari ya Kigoma ambayo inahusisha bandari zote zilizopo katika Ziwa Tanganyika, imeanza kufanyiwa maboresho kuanzia mwaka 2016/17 ikihusisha ujenzi wa magati, ununuzi wa mitambo, ujenzi wa maghala na majengo ya abiria pamoja na ujenzi wa ofisi za kisasa za makao makuu ya Bandari hiyo ambazo ziko katika hatua za mwisho kukamilika.

Aliongeza kuwa maboresho hayo yanafanyika kutokana na kasi kubwa ya ongezeko la mahitaji ambayo hayakuendana na miundombinu iliyokuwapo awali.

Alisema bandari za Ziwa Tanganyika zimekuwa kiungo kikubwa cha biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Burundi na Zambia, huku biashara kubwa ikiwa ni mazao yanayozalishwa Tanzania.

Kakoko alisema bandari hizo zimekuwa kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wa wananchi wa mikoa inayozunguka Ziwa Tanganyika kutokana mazao yao kupata idadi kubwa ya wanunuzi wanaotokana na kutumia bandari hiyo.

Pia, alisema matumizi ya bandari pamoja na meli katika usafirishaji, kumesaidia kupunguza bei za bidhaa ambazo gharama zake zimekuwa zikipanda kutokana na gharama kubwa za usafirishaji.

Kakoko alisema bado kuna maboresho zaidi yanaendelea katika bandari Kuu ya Kigoma yanayohusisha ujenzi wa gati ya maboti ya Kibirizi, gati ya abiria na makasha pamoja na ujenzi wa bandari Kavu ya Katosho.

# Waridhishwa ofisi TBS kwenye kanda

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI wamepongeza uamuzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kufungua ofisi za kanda, wakisema zimewarahisishia kupata huduma ikiwamo uthibitishaji ubora wa bidhaa wanazozalisha bila kulazimika kufunga safari hadi makao makuu ya shirika hilo, jijini Dar es Salaam.

Walitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza kwenye Maonyesho ya Bidhaa za Viwanda vya Wanawake Tanzania yaliyoandaliwa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC).

Maonyesho hayo yaliyoanza Februari 26, yalimalizika jana kwenye Viwanja vya Posta, Kijitonyama jijini Dar es Salaam.

Mmiliki wa Kampuni ya RUMZAHRAIM Investment ya mkoani Mtwara, Rikia Liumba, alisema TBS kufungua ofisini kwenye kanda imewafanya wawe karibu na shirika hilo.

Alitoa mfano kuwa siku za karibuni alikumbana na changamoto kwenye uzalishaji wa bidhaa zake, lakini kwa sababu TBS wapo Mtwara ilikuwa rahisi kwake kuwafuata na kumsaidia tatizo lake. Akieleza faida alizopata tangu alipopatiwa leseni ya kutumia alama ya ubora wa TBS, tangu Agosti, mwaka jana alisema bidhaa yake ya unga wa muhogo imezidi kupata soko kinyume na hapo awali.

Alisema wanapothibitisha bidhaa zao wanakuwa wameondokana na vikwazo vya kibiashara, kwani zamani unga wake ulikuwa unakataliwa kwenye masoko makubwa, lakini sasa hivi wanamtafuta mwenyewe.

Alisema kabla ya kwenda TBS kupata alama ya ubora alienda SIDO ambao walikuwa wakimpatia elimu kuhusu uzalishaji bidhaa zake na baadaye aliwaomba wamuunganishe na shirika hilo aweze kuthibitisha bidhaa zake.

Mjasiriamali mwingine, Anna John, alisema changamoto ambazo alikuwa akikumbana nazo kabla ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zake, kwa sasa zimegeuka fursa.

Akizungumza ushiriki wa TBS kwenye maonesho hayo, Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Frola Luvanda, alisema walishiriki maonesho hayo kwa ajili ya kutoa elimu kwa wajasiriamali kuhusu umuhimu wa kuthibitisha bidhaa zao.

Alisema kwenye maonesho hayo wanashiriki wajasiriamali ambao wamethibitisha bidhaa zao, wengine wapo kwenye mchakato huo na wapo ambao bidhaa zao hazijathibitishwa.

# Waganga waagizwa kutoa elimu ya lishe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewaagiza waganga wakuu wa mikoa na maofisa ustawi wa jamii, kuhakikisha wanajenga utaratibu wa kukutana na mamalishe, wajasiriamali na vikundi mbalimbali kuwapa elimu ya namna ya kuandaa lishe bora ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko.

Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Elimu kwa Umma wa Wizara ya Afya, Dk. Ama Kasangala, aliyasema hayo alipokuwa akifungua tamasha la wanawake lililoandaliwa na Shirika linalojihusisha kutoa msuk mo kwa jamii katika mapambano ya Maendeleo (CFCTO).

Dk. Kasangala alisema lengo la Wizara ni kuhakikisha jamii inafuata taratibu za kujikinga na magonjwa mbalimbali, ndio maana kitengo hiko kimekuwa kikitoa elimu ya namna ya kujikinga na magonjwa mbalimbali yakiwamo ya mlipuko.

Alivishukuru vikundi mbalimbali vya mkoa wa Dodoma, kutokana na kuitikia wito wa kupata elimu hiyo, ambayo iliendana sambamba na ufanyaji mazoezi ili kuuweka mwili sawa jambo ambalo linasaidia kuwa na afya bora.

Naye, Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Endless Success Foundation, Amina Ferus, alisema lengo la kukutana pamoja ni kuamsha uelewa na kuiwezesha jamii katika kutokomeza umaskini, ujinga na kupeana elimu ya namna ya kujikinga na magonjwa mbalimbali.

Nipashe
Spotika




NYOTA 10 WA AFRIKA WENYE THAMANI ZAIDI DUNIANI 2021 UK. 12-13




# WACHEZAJI 5 WAINGEREZA WANAONG'ARA NJE YA EPL

SANCHO

**LONDONA,** England

WAKATI wachezaji kutoka Ulaya wamejaa kwenye Ligi Kuu England tangu maboresho ya ligi hiyo mwaka 1990, wachezaji wa Uingereza walikuwa wachache sana wanaokwenda kucheza ligi za nchi nyingine. Hata hivyo, hivi sasa mambo yamebadilika.

Wachezaji wengi Waingereza wameamua kwenda kucheza nje kwa kipindi cha misimu michache iliyopita. Wachezaji kama Kieran Trippier, Chris Smalling na Ashley Young wamehama na kwenda kucheza kwenye ligi nyingine Ulaya.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano Waingereza wanaofanya vizuri nje ya Ligi Kuu England, twende sasa...

**#1. JADON SANCHO (BORUSSIA DORTMUND)**

Pengine ni haki kusema kwamba, Jadon Sancho kwa sasa ndiye amewahamasisha zaidi wachezaji wa Uingereza kucheza nje ya EPL.

Winga huyo aliondoka Manchester City na kwenda Borussia Dortmund wakati akiwa na umri wa miaka 17 kipindi cha majira ya joto mwaka 2017. Na tangu hapo amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Msimu wa 2018-19, alicheza mechi 34 za Bundesliga akifunga mabao 12 na pasi za mwisho 14 na mwaka 2018, akaitwa kwa mara ya kwanza kikosi cha timu ya Taifa ya England.

**#2. STEPHY MAVIDIDI (MONTPELLIER)**

Arsenal ni klabu inayoheshimika kwa kuwaruhusu vijana wengi kama Serge Gnabry na Wojciech Szczesny kwenda kutafuta mafanikio zaidi nje ya Emirates katika miaka ya hivi karibuni.

Huyu ni straika wa timu ya Taifa ya England akiwa amehitimu kwenye akademi ya vijana ya Arsenal alikokaa miaka nane na aliondoka mwaka 2018 akiwa na umri wa miaka 20 na kwenda kujiunga na miamba wa Italia, Juventus.

Licha ya kuwa Muingereza wa kwanza kuichezea Juventus tangu David Platt, Mavididi hakufanikiwa pale Turin.

Lakini badala ya kurudi England, akaamua kwenda nchini Ufaransa na akajiunga na Dijon, ambako alifunga mabao matano kwenye mechi 24 msimu wa 2019-20.

Kipindi cha majira ya joto mwaka 2020, akahamia Montpellier kwa ada ya euro milioni sita na tangu hapo amekuwa na kiwango cha kuvutia.

Mavididi amejiimarisha yeye mwenye kama mmoja wa wachezaji wa kikosi cha kwanza cha kocha Michel de Zakarian akicheza mechi 23 za Ligue 1.

**#3. ANGEL GOMES (BOAVISTA)**

Angel Gomes amekuwa moto kule Boavista tangu alipoondoka Manchester United kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Mwaka 2017, Gomes alitengeneza historia wakati alipokuwa mchezaji wa kwanza kijana zaidi kuichezea Manchester United na kuwa mchezaji wa kwanza aliyezaliwa mwaka 2000 kucheza Ligi Kuu England.

Hata hivyo, hakuwa na nafasi kwenye kikosi cha kwanza na kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2020, aliondoka pale Old Trafford.

Alisajiliwa na Lille kwa mkataba wa miaka mitano na wakamtoa kwa mkopo katika klabu ya Boavista ya nchini Ureno mwanzoni mwa msimu huu wa 2020-21. Na amekuwa kwenye kiwango bora zaidi akitoa pasi za mwisho mbili katika mechi mbili na kufunga bao moja.

**#4. NONI MADUEKE (PSV EINDHOVEN)**

Jina la Noni Madueke limekuwa likitamba kwenye Ligi Kuu Uholanzi. Alitokea akademi ya Tottenham na sasa akiwa na umri wa miaka 18, amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia pale PSV Eindhoven tangu alipojiunga nayo kipindi cha majira ya joto mwaka 2018.

**#5. JUDE BELLINGHAM (BORUSSIA DORTMUND)**

Baada ya mafanikio ya Jadon Sancho, ambaye alihamia Borussia Dortmund mwaka 2017, ilionekana ni wazi kwamba miamba hao wa Bundesliga wangewasajili wachezaji wengi kutoka Uingereza.

Na Julai 2020, wazo hilo likaja wakati walipoilipa Birmingham City pauni milion 25 na kumtwaa kiungo Jude Bellingham - na kumfanya kuwa mchezaji ghali zaidi mwenye umri wa miaka 17 katika historia ya soka la Uingereza.

Bellingham amecheza mechi 41 kwa Birmingham msimu wa 2019-20, na alipouzwa klabu hiyo ilistaafisha jezi yake namba 22.

Bellingham bado hajafikisha umri wa miaka 18 hadi Juni, lakini tayari amecheza mechi 18 za Bundesliga pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Bellingham tayari ameshaichezea timu ya taifa ya wakubwa ya England.

## ISIKUPITE

GEORGE Weah ambaye kwa sasa ni Rais wa Liberia, bado anaendelea kushikilia rekodi ya kuwa Mwafrika aliyefunga mabao mengi Ligi Kuu Italia Serie A akiwa na mabao 46, akifuatiwa na Gervinho (Ivory Coast- mabao 39), Khouma Babacar (Senegal- mabao 39), Mohamed Kallon (Sierra Leone- mabao 39) na Keita Balde (Senegal, mabao 36).



# NYOTA 10 WA AFRIKA WENYE THAMANI ZAIDI DUNIANI 2021

**LONDON,** England

AFRIKA imezalisha wachezaji wengi wenye vipaji vya hali ya juu kwa kipindi cha miongo minne iliyopita. Wengi wa nyota hao wamekuwa wakicheza zaidi katika nafasi ya ushambuliaji.

**Hata hivyo, kwa sasa pia kuna walinzi na magolikipa kutoka bara hili na wanang'ara kwenye ligi mbalimbali duniani.**

Samuel Eto'o, George Weah, Didier Drogba, Roger Milla na Yaya Toure ni baadhi ya wachezaji ambao wameitangaza Afrika vizuri sana, kitu ambacho kinashangaza ni kwamba hadi sasa ni nyota mmoja tu kutoka bara hili ambaye amewahi kutwaa taji la Ballon d'Or. Nyota huyo ni Weah ambaye kwa sasa ni rais wa Liberia.

Makala haya inawaangalia wachezaji 10 ambao wana thamani kubwa zaidi duniani kwa sasa, twende sasa...

### #10. WILFRED NDIDI – EURO MIL. 45

Wilfred Ndidi alikuwa nguzo kubwa wakati Leicester City ikifuzu kucheza Ligi ya Europa msimu uliopita. Raia huyo wa Nigeria ni mmoja wa viungo bora zaidi wakabaji barani Ulaya kwa wakati huu.

Euro milioni 20 iliyolipwa kwa Genk mwaka 2017 sasa inaonekana kama ni ndogo sana. Kwani thamani yake kwa sasa ni euro milioni 45.

### #9. HAKIM ZIYECH – EURO MIL. 45

Morocco ina kikosi imara sana kwa sasa, hasa linapokuja suala la idara ya ushambuliaji. Mmoja wa nyota wanaotamba kwa Simba hao wa Atlas ni Hakim Ziyech.

Straika huyo alitengeneza jina lake mwenyewe wakati akiwa kwenye kikosi cha Ajax kilichokuwa na nyota kama Matthijs De Ligt, Donny Van de Beek na Frenkie De Jong.

Kikosi kile cha vijana kiliwafunga Real Madrid na Juventus kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kufuzu nusu fainali msimu wa 2018-19.

Kiwango chake kikamfanya apate nafasi ya kusajiliwa Chelsea Februari 2020 na sasa thamani yake imepanda na kuwa euro milioni 45.

### #8. RIYAD MAHREZ – EURO MIL 48

Algeria kwa sasa ndio mabingwa wa Afrika, wakiwa wameshinda taji hilo kwenye mashindano yaliyofanyika nchini Misri mwaka 2019. Hivyo, ilitarajiwa kwamba wachezaji wengi kutoka kwa kikosi hicho cha 'Mbweha wa Jangwani' kuwapo kwenye orodha hii. Chakushangaza ni nahodha, Riyad Mahrez pekee ndio yupo.

Winga huyo wa Manchester City amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu England, licha ya kutopata nafasi chache za kucheza chini ya kocha Pep Guardiola.

Bado hajawa kwenye kiwango alichokionyesha kule Leicester alipoisaidia kutwaa taji la Ligi Kuu msimu wa 2015-16. Alitimiza umri wa miaka 30 mwezi huu na thamani sasa ni euro milioni 48.

### #7. VICTOR OSIMHEN – EURO MIL 50

Victor Osimhen mara kwa mara anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji wenye vipaji vikubwa kutoka Afrika. Tayari ameshafungua akaunti ya mabao kule Napoli, klabu aliyojiunga nao mwanzoni mwa msimu huu, na ana mabao mawili kwa jina lake katika mashindano yote.

Amekuwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Nigeria tangu mwaka 2017 na amecheza mechi 10 kwa Nigeria, na amefunga mabao manne. Mabao yake yote aliyafunga miaka miwili iliyopita. Kwa sasa thamani yake ni euro milioni 50.

### #6. ACHRAF HAKIMI - EURO MIL. 50

Katika soka la kisasa mabeki wa pembeni ni muhimu sana. Anakipiga pale Inter Milan nafasi ya beki wa kuli na kwa sasa ni mmoja wa walinzi bora zaidi barani Ulaya kwa nafasi hiyo na amefiti vizuri katika mfumo wa kocha Antonio Conte.

Thamani yake imepanda kutoka euro milioni 40 ambazo Inter walilipa kwa Real Madrid hadi euro milioni 50 kwa sasa. Pia ni mmoja wa walinzi wenye thamani kubwa Afrika.

### #5. THOMAS PARTEY - EURO MILIONI 50

Thomas Partey ni mchezaji mwingine ambaye msimu huu anacheza katika timu mpya na ni raia wa Ghana pekee katika orodha ya wachezaji wenye thamani kubwa kutoka Afrika.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, alisaini kuichezea Arsenal mwanzoni mwa msimu huu akitokea Atletico Madrid, huku Lucas Torreira akienda upande mwingine.

Majeruhi yamemfanya kukosa mechi nyingi za Ligi Kuu msimu huu, lakini thamani yake kwa sasa ni euro milioni 50.

### #4. WILFRED ZAHA – EURO MIL. 50

Kujumuishwa kwa Wilfred Zaha kwenye orodha hii pengine kutawashangaza mashabiki wachache wa Ligi Kuu England. Nyota huyo wa Crystal Palace aliichezea timu ya taifa ya vijana ya England chini ya umri wa miaka 19 na 21, lakini baadaye mwaka 2017 akaamua kuichezea Ivory Coast, sehemu ambayo alizaliwa.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester United ni mmoja wa mastraika wenye kiwango cha kuvutia.

Katika umri wake wa miaka 28, yupo kwenye kiwango cha juu, ingawa amekuwa akikabiliwa na majeraha ya mara kwa mara. Thamani yake ya sasa inatajwa kuwa ni euro milioni 50.

### #3. KALIDOU KOULIBALY – EURO MIL. 60

Walinzi thamani yao imekuwa ikipanda kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita. Wachezaji kama Virgil Van Dijk wamethibitisha namna gani walivyoimara kwenye safu ya ulinzi wa kati.

Kalidou Koulibaly ni mmoja wa walinzi ambao wapo kwenye kiwango bora zaidi kwa sasa. Alikuwa nguzo ya Napoli wakati wakishinda taji la Coppa Italia msimu uliopita.

Yeye ni miongoni mwa kikosi imara cha Senegal, na sasa thamani yake inatajwa kuwa euro milioni 60.

### #2. SADIO MANE – EURO MIL. 120

Liverpool ni moja ya timu yenye kikosi imara zaidi duniani kwa sasa, ikiwa imetinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita na wakitwaa Kombe la Ligi msimu uliopita.

Sadio Manea amechomoza kama mmoja wa mawinga bora duniani pale Liverpool na ukiangalia nyuma ada ya euro milioni 40 iliyolipwa mwaka 2016, sasa ni tofauti kabisa.

Yupo msimu wake wa tano na klabu hiyo na tayari ameshinda mataji manne na 'Wekundu' hao. Pia aliisaidia Senegal kutinga fainali ya mataifa ya Afrika mwaka 2019.

Msimu wa 2019-20 ulikuwa bora zaidi kwake, lakini msimu huu amekuwa kwenye kiwango kisicho bora zaidi.Amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kuhamia Real Madrid kwa kipindi cha mwaka uliopita. Na sasa thamani yake inatajwa kuwa euro milioni 120.

### #1. MOHAMED SALAH – EURO MIL. 120

Mara kwa mara amekuwa akiitwa 'Messi wa Afrika', Mo Salah ni mmoja wa wachezaji bora duniani kwa sasa. Winga huyu wa Misri amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu aliposajiliwa na kocha Jurgen Klopp pale Liverpool mwaka 2017.

Tayari amefikisha mabao 100 kwa 'Wekundu' hao, na kuwa mchezaji pekee kufikia idadi hiyo ya mabao tangu gwiji Steven Gerrard.

Kwa sasa yupo kwenye msimu wake wa nne na klabu hiyo na tayati ameshinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu mara mbili na anaongoza kwa kufunga mabao kwenye Ligi Kuu England msimu huu 2020-21.

Mchezaji huyo alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi pale Merseyside, kwa euro milioni 42 mwaka 2017. Na sasa thamani yake inatajwa kuwa euro milioni 120.




MANE

## Nukuu

"Ukisoma namba hizi kwa sauti kubwa basi inaonekana sio, lakini hatupaswi kupunguza mawazo yetu. Tunapaswa kujaribu na sio kujiandaa kwa visingizio. Kiasi cha alama kinaonyesha jinsi pengo lilivyo kubwa, lakini lazima iwe matarajio ya kuipunguza haraka iwezekanavyo," **Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel, akiamini bado wana nafasi ya ubingwa Ligi Kuu England.**



"Bado tuna nafasi kwenye mbio za ubingwa. Najua vijana hawa wanaamini, wanafanya mazoezi vizuri na wanataka kurudi kushinda taji na hii inanifanya nijisikie raha, hatuangalii ni nani aliye juu yetu au nyuma yetu, tunakazana sisi wenyewe. Lengo lazima libaki vile vile. Kuna michezo mingi bado, tutakuwapo,"**Kocha wa Juventus, Andrea Pirlo.**



"Hatufungi mabao yakutosha, hilo ni kwa uhakika kabisa, tunatakiwa kushinda, kupata mabao na kuondoka na pointi tatu," **Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer.**



# SIMBA, WYDAD NA REKODI YA NYAVU ZISIZOTIKISWA CAF



Kiungo wa Simba, Rally Bwalya, akiwatoka mabeki wa Al-Merreikh kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Jumamosi iliyopita nchini Sudan na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: SIMBA**

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, ni moja kati ya timu mbili tu kati ya 16 ambazo zinazoshiriki ligi hiyo ambazo hajjaruhusu bao lolote mpaka sasa wakati mzunguko wa kwanza uliisha juzi kwa kila timu kucheza mechi tatu.

Baada ya juzi Jumamosi kulazimisha suluhu ugenini dhidi ya Al-Merreikh ya Sudan, Simba imeingia kwenye rekodi hiyo pamoja na Wydad Casablanca ya Morocco ambayo nayo siku hiyo, ikiwa nyumbani iliikandamiza Horoya ya Guinea mabao 2-0 na kuendelea kuliongoza Kundi C ikiwa nayo haijaruhusu bao lolote.

**Timu 14 zilizobaki zote tayari nyavu zao zimeshatikiswa kwenye michuano hiyo mikubwa barani Afrika.**

Simba yenyewe ni kinara ya Kundi A, ikiwa na pointi saba, ikiziongoza timu za AS Vita ya DR Congo yenye pointi nne, sawa na Mabingwa Watetezi Afrika, Al Ahly ya Misri, yenye pointi nne pia, huku Al-Merreikh ya Sudan, ikishika mkia kwa pointi moja.

Wydad, ina pointi tisa, inaziongoza timu za Horoya ya Guinea na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini zote zikiwa na pointi nne, huku Petro Atletico ya Angola ikiwa haina pointi yoyote mpaka sasa.

Katika makala haya, tunakuletea takwimu za timu zote ambazo zimeruhusu mabao na ambazo hazijaruhusu kwenye hatua hii ya makundi msimu huu, tiririka nayo sasa...

**#1. SIMBA - KUNDI A (HAIJARUHUSU BAO)**

Simba imemaliza mzunguko kwa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiweka rekodi ya kutoruhusu bao lolote mpaka sasa, ikicheza mechi tatu mbili za ugenini na moja nyumbani.

Ikiwa ugenini DR Congo, ilishinda bao 1-0, ikarejea Dar es Salaam na kuwachapa Mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri bao 1-0, kabla ya kwenda kutoa suhulu ya bila kufungana dhidi ya Al-Merreikh ya Sudan, ikimaliza mzunguko wa kwanza ikiwa na mabao mawili na haijafungwa.

**#2. WYDAD CASABLANCA - KUNDI C (HAIJARUHUSU BAO)**

Timu hii ya nchini Morocco, kama Simba, haijaruhusu bao lolote mpaka sasa. Mbali na hilo, imeshinda mechi zote tatu ilizocheza.

Ilianzia ugenini nchini Angola dhidi ya Petro Atletico ikashinda bao 1-0, ikarudi nyumbani na kucheza mechi mbili, ikiibabua Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini mabao 4-0 na juzi Jumamosi ikiichapa Horoya mabao 2-0.

**#3. MC ALGER - KUNDI D (BAO 1)**

MC Alger ya Algeria, timu ambayo iko kwenye Kundi C, inaonekana nayo ina ukuta mgumu kwani mpaka sasa imeruhusu bao moja tu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

Inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi tano nyuma ya Esperance ya Tunisia inayoongoza kundi hilo ikiwa na pointi saba. Ilitoa suluhu na Zamalek ya Misri, ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Esperance, kabla ya kushinda1-0 dhidi ya Teungueth ya Senegal.

**#4. MAMELODI SUNDOWNS - KUNDI B (BAO 2)**

Vinara wa Kundi B, Mamelodi Sondowns ya Afrika Kusini, yenyewe inaliongoza kundi hilo, ikiwa na pointi tisa na mabao ya kufunga tisa, lakini imeruhusu mabao mawili mpaka sasa, nayo pia ikiwa imeshinda mechi zake zote tatu ilizocheza.

**#5. TP MAZEMBE - KUNDI B (BAO 2)**

Baada ya kuchapwa mabao 2-1 nyumbani dhidi ya Mamelodi Sundowns Jumamosi iliyopita, TP Mazembe ya DR Congo, inashika nafasi ya tatu kwenye Kundi B kwa pointi mbili baada ya mzunguko wa kwanza, lakini nayo ikiwa imesharuhu mabao mawili.

**#6. HOROYA - KUNDI C (BAO 2)**

Kwenye Kundi C, Horoya ya Guinea inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne nyuma ya Wydad Casablanca. Nayo mpaka sasa imeruhusu mabao mawili kwenye nyavu zake.

**#7. AL AHLY - KUNDI A (MABAO 3)**

Mabingwa Watetezi, Al Ahly ambao wanakamata nafasi ya tatu kwenye Kundi A, linaloongozwa na Simba, tayari wamesharuhusu nyavu zao kutikishwa mara tatu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

**#8. AL HILAL OMDURMAN - KUNDI B (MABAO 3)**

Timu hii ya Sudan, mpaka sasa ipo kwenye nafasi ya pili ya Kundi B, juu ya TP Mazembe zote zikiwa na pointi mbili. Hata hivyo, Al Hilal mpaka sasa imeruhusu mabao matatu kwenye nyavu zake.

**#9. ESPERANCE - KUNDI D (MABAO 3)**

Vinara wa Kundi D, Esperance ya Tunisia, wana pointi saba mpaka sasa, wakiwa wamefunga mabao sita, lakini nao pia wameruhusu mabao matatu mpaka sasa.

**#10. ZAMALEK - KUNDI D (MABAO 3)**

Wamisri hawa wamemaliza mzunguko wa kwanza wakishika nafasi ya tatu Kundi D kwa pointi mbili, pia wameshafungwa mabao matatu mpaka sasa.

**#11. TEUNGUETH - KUNDI D (MABAO 3)**

Hii ni timu kutoka Senegal ambayo inaburuza mkia kwenye Kundi D kwa kuwa na pointi moja tu. Hata hivyo imepachikwa mabao matatu mpaka sasa.

**#12. AS VITA - KUNDI A (MABAO 4)**

Inakamata nafasi ya pili kwenye Kundi A nyuma ya Simba ikiwa na pointi nne. Imefunga mabao sita mpaka sasa, lakini imesharuhsu mabao manne nyavuni.

**#13. KAIZER CHIEFS - KUNDI C (MABAO 4)**

Timu hii kutoka Afrika Kusini, iko kwenye nafasi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi nne, lakini pia imeruhusu mabao manne mpaka sasa.

**#14. PETRO ATLETICO - KUNDI C (MABAO 5)**

Inashika mkia kwenye Kundi C. Timu hii kutoka Angola, Haina pointi na imeruhusu mabao matano mpaka sasa kwenye kundi lake.

**#15. CR BELOUZDAD - KUNDI B (MABAO 6)**

Ni timu kutoka Algeria ambayo inazibeba timu zote za Kundi B. Ina pointi mbili na imeruhusu mabao sita mpaka sasa kwenye vyavu zake.

**#16. EL MERREIKH - KUNDI A (MABAO 7)**

Timu hii ya Sudan ambayo ipo Kundi A linaloongozwa na Simba, inakamata mkia ikiwa na pointi moja, lakini ndiyo timu inayoongoza kwa kufungwa mabao mengi mpaka sasa kwenye ligi hiyo kwa makundi yote manne. Imeruhusu mabao saba.

**JE, WAJUA?**



MABAO mawili aliyofunga Erling Braut Haaland wakati Borussia Dortmund ikichezea kichapo cha 4-2 dhidi ya Bayern Munich juzi, yamemfanya kuwahi kufikisha mabao 100 kwenye mashindano yote tangu aanze kucheza timu ya wakubwa, kwa sasa akiwa na umri wa miaka 20, imemchuakua mechi 145 kufikisha idadi hiyo - ukilinganisha na Kylian Mbappe yeye ilimchukua mechi 180, Lionel Messi (mechi 210) na Cristiano Ronaldo (mechi 301).



# Wanawake viongozi shupavu wafundwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAWAKE viongozi wameaswa kutosahau majukumu yao ya kifamilia wanapoonyesha ushupavu wa uongozi kwenye maeneo ya kazi.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ( UCSAF), Justina Mashiba. alitoa rai hiyo juzi wakati wanawake wa mfuko huo wakitoa msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh.Milioni 4.5 kwa kituo cha kulelea watoto yatima cha Nyumba ya Matumaini jijini hapa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani leo.

Mashiba alisema wanawake hasa viongozi wanapaswa kuwa wabunifu na kufanya kazi kwa uadilifu na ufanisi mkubwa huku wakiendelea kutambua kuwa wao ni wazazi na walezi wa familia.

Alisema ili taifa liendelee kuwa na watoto waliolelewa katika misingi bora ya kifamilia, wanawake hasa viongozi wanatakiwa kutambua kuwa nafasi za uongozi walizonazo si mbadala wa majukumu yao katika familia.

"Nitoe wito kwa wanawake wenzangu hasa viongozi unapokuwa katika majukumu ya kikazi kuonyesha ushupavu wako lakini unaporudi nyumbani usiwe kiongozi wa baba timiza majukumu yako kama mwanamke, wewe ni mama, tusilisahau hilo,"alisema.

Aidha, Mtendaji huyo alisema baadhi ya familia zimekuwa kwenye migogoro ambayo inasababisha unyanyasaji na kutengana kwa wazazi hali ambayo inachangia ongezeko la watoto yatima pamoja na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi.

"Sisi wanawake wa UCSAF tumeona tutoe kile tulichojaliwa kwa ajili ya kuwajali watoto hawa na kumshukuru Mungu kwa nafasi hizi za uongozi ili tuwajali wenye uhitaji kama hawa watoto yatima,"alisema.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Sista Aurea Kyara, alisema kituo hicho kina watoto zaidi ya 70 na kuushukuru mfuko huo kwa msaada.

Alitoa wito taasisi na wadau wengine kuendelea kujitolea katika kusaidia kituo hicho pamoja na vituo vingine vinavyolea yatima.

"Tatizo lililopo baadhi ya ndugu wa watoto hawa huwatelekeza baada ya kuwaleta kituoni baada ya wazazi kufariki dunia, pia baadhi ya watoto wamekuwa wakikataa kurudi kwenye familia zao muda unapofika, hali ambayo inasababisha kituo kuendelea kuwa na idadi kuwa ya watoto," alisema.



Ofisa wa ardhi wa Jiji la Dodoma, Leonard Machunde, akijibu kero mbalimbali kutoka kwa wananchi wa Mtaa wa Ndachi Kata ya Mnadani jijini Dodoma, kwenye mkutano uliofanyika juzi ambapo walidai kucheleweshewa upimaji wa viwanja na utoaji wa vibali kwa ajili ya kujenga nyumba. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# LITA yatakiwa kuzingatia uadilifu, maadili

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, ameitaka Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kuzingatia maadili na uadilifu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Prof. Ole Gabriel alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifungua mkutano wa Baraza la Nane la Wafanyakazi wa Taasisi hiyo.

Alisema mikutano ya aina hiyo inapaswa kuwa na tija kwa watumishi na watu wote wanaonufaika na uwepo wa taasisi hiyo.

"Mkutano huu ni mkubwa sana na una heshima yake hivyo ni vizuri utumike kujadili kwa kina namna ya kupunguza na kuondoa kero za watumishi wa kampasi zote za LITA ili kutekeleza vyema jukumu la kuzalisha wataalam wa tasnia ya ufugaji hapa nchini," alisema.

Alitoa wito kwa kampasi zote za taasisi hiyo kuhakikisha zinabadilisha mifumo yake ya ufundishaji ili kuwafanya wahitimu wa vyuo hivyo kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa kama ilivyozoeleka hivi sasa.

"Huwa inanisikitisha sana kumuona mzazi anamgharamia mwanae ada ya masomo kwa miaka isiyopungua mitatu halafu baadae mzazi huyo huyo anaanza kuwajibika kumtafutia mtoto wake ajira, ni lazima tubadilishe huu mtazamo na kwa sababu chuo chenu kimejikita zaidi kwenye vitendo ni wakati sasa mzalishe wataalam watakaojitegemea kwenye soko la ajira," alisema.

Aliitaka LITA kuhakikisha inazingatia usawa wa kijinsia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ndani ya taasisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi wanawake katika ngazi mbalimbali wanazostahili.

"Kuwa mnene au mwembamba ni juhudi za mtu binafsi, lakini kuwa mwanamke au mwanaume ni uamuzi wa Mungu hivyo si vyema kushindwa kumpa mtu nafasi kisa ni mwanamke na kufanya hivyo kwa kweli ni kosa kubwa sana," alisema. Awali, akitoa taarifa ya utangulizi kuhusu mafanikio ya LITA, Mtendaji Mkuu wa wakala huo, Dk. Pius Mwambene, alisema katika kipindi cha mwaka uliopita wakala umefanikiwa kuongeza nafasi ya udahili wa wanafunzi kutoka 2,536 hadi 3,574 mwaka huu.

"Hata hivyo kutokana na ongezeko hilo, tumekuwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na mabweni, madarasa, maabara, maktaba na walimu wa fani za afya ya Mifugo na uhandisi kilimo ambapo mpaka sasa tunahitaji walimu 34," alisema.

Aidha Dk. Mwambene alisema wanakabiliwa na tatizo la uchakavu ikiwa ni pamoja na majengo ambayo kwa sehemu kubwa yanatakiwa kuvunjwa na kujengwa mengine.

# Miti 8,000 kuifanya Dodoma ya kijani

**Na Peter Mkwavila** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali ya Rafiki Wildlife Foundation (RWF) kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) imetoa zaidi ya miti 8,000 kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma ili kuufanya kuwa wa kijani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Mchungaji Clement Matwiga, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza kwenye upandaji wa miti uliofanyika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha DECCA, kilichopo Nala na Chuo Kikuu cha Kanisa la TAG (Central Bible College-Dodoma).

Mchungaji Matwiga alisema kuwa wametoa miti hiyo ikiwa ni juhudi za kuunga mkono serikali pamoja na kufanya uendelezaji wa Dodoma kuwa ya kijani sambamba na kuenzi siku ya wanyama Duniani ambayo hufanyika Maschi 3, kila mwaka.

Alisema miti hiyo itasaidia kutunza wanyama kwa kuwa kama hakuna mazingira mazuri yanayowavutia wanyama wa aina zote ni vigumu kutunza wanyama.

"Mimi kama Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Rafiki Wildlife Faundation, kwa kushirikiana na wakala wa misitu pamoja na wadau mbalimbali wa mazingira tumeona kuna umuhimu wa kutoa miti katika mashirika na taasisi mbalimbali kwa kuhamasisha mazingira kwa lengo ya kuyaboresha na kuyapendekeza," alisema.

Akipokea miti hiyo, Mkuu wa Chuo cha DECCA, Dk. James Ng'wandu, alisema upandaji miti Mkoa wa Dodoma ni uendelezaji wa kutimiza azma ya serikali ya kuhimiza kufanya mazingira kuwa mazuri.

Naye, Mratibu wa Dodoma ya Kijani, TFS, Frank Chambo alisema wataendelea kuhamasisha upandaji wa miti ikiwa na utunzaji wa mazingira.

"Tumekuwa tukiwahamasisha Watanzania pamoja na taasisi zote za umma, serikali na watu binafsi kuhakikisha wanapanda miti ya aina mbalimbali ikiwamo ya vivuli, matunda na miti tiba," alisema.

Alisema kuna mikakati ya muda mrefu kwa Dodoma ili kuondokana na dhana iliyojengeka kuwa Dodoma ni kame.

Davidi Mwakipesile ambaye ni Meneja wa Kitengo cha Mahusiano Kampuni ya Grumeti Fund iliyoko Wilaya ya Serengeti, alisema kuwa kwa sasa kampuni hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na elimu inayotolewa kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira.

Alisema kuwa hivi sasa jamii ambayo imezunguka kwenye uhifadhi imekuwa na uelewa wa maendeleo katika kuhakikisha wanawatunza wanyama wanaotoroka kuingia kwenye makazi na kuwalinda.





Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kifua kikuu na dawa za kulevya, Fatma Toufiq (kulia), akikagua bidhaa mbalimbali ambazo zinazalishwa na vikundi vya watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) jijini Mbeya, wakati kamati hiyo ilipotembelea Konga ya Jiji la Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wabeba maiti, wagonjwa kwenye machela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata za Maendeleo na Tembela katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanalazimika kusafirisha maiti kwa kutumia machela kutokana na barabara inayounganisha kata hizo kuharibika, hivyo kusababisha magari na vyombo vingine vya moto kushindwa kupita.

Aidha, wananchi wa kata hizo wanadai kuharibika kwa barabara hiyo kuwalazimu kubeba maiti na wagonjwa kwa kutumia machela pamoja na kushindwa kusafirisha mazao yao kwenda sokoni hasa viazi mviringo ambavyo ndio zao kuu la biashara kwenye maeneo hayo.

Wakizungumza na wandishi wa habari juzi, walidai wamekosa mawasiliano ya barabara hasa kipindi hiki ambacho mvua inanyesha, huku baadhi ya wanawake wakidai wanalazimika kujifungulia njiani.

Diwani wa Kata ya Maendeleo, Daniel Nyamwale, alisema barabara hiyo ya Simambwe-Shamwengo ina urefu wa kilomita 27, na kwamba kwa sasa tatizo kubwa lipo kuanzia katika Kijiji cha Muungano mpaka Shamwengo.

Alisema mbali na barabara kuharibika, pia daraja la Mto Mawe lina hatarisha maisha ya wananchi kutokana na kutokuwa na kingo upande mmoja na hivyo kuwa hatari kwa mtu yeyote ambaye atateleza.

Aliiomba Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na vijijini (TARURA) kuikarabati barabara hiyo ili wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo.

"Daraja la Mto Mawe mawasiliano yamekatika, sasa mtu akifa mjini tunasafirisha kwa gari mpaka hapa kisha tunafunga kwenye machela na kubeba 'mzega mzega' mpaka nyumbani, hili ni tatizo kubwa sana kwetu tunaiomba Serikali itusaidie," alisema Nyamwale.

Kwa maeneo yaliyoharibika ambayo ni Daraja la Mto Mawe na eneo la Shilabhi yana urefu wa kilomita moja, hivyo aliiomba Serikali kukarabati kipande hicho kwa bajeti ya dharura, huku akiomba baadaye itengwe bajeti ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe ili ipitike mwaka mzima.

Naye Diwani wa Tembela, Juma Mwakalobo, alisema wanalazimika kushusha maiti katika Kijiji cha Simambwe na kuanza kusafirisha kwa machela.

Alisema barabara hiyo ni hatari kutokana na kuwa na milima na madaraja, na kwamba baadhi ya magari huwa yanashindwa kupanda milima na kuanza kurudi nyuma, hali ambayo huwa inahatarisha maisha ya watu.

Alisema katika daraja la Mto Mawe, kuna mwananchi amewahi kuangukia mtoni kutokana na daraja hilo kutokuwa na kingo, na kwamba wananchi wamekuwa wakilalamika mara kwa mara.

"Mimi mwenyewe nilishuhudia wananchi wakiwa wamembeba mjamzito kwenye machela, walinikuta kwenye makao makuu ya kata, niliumia sana, maana yule mama alikuwa amechoka sana, pengine ningekuwa na kamera ningepiga picha, maana haya mambo ni ya zamani sana," alisema Mwakalobo.

Nao baadhi ya wanawake walisema kitendo cha kubebwa kwenye machela kinawakera na kuwaumiza, na kwamba hakuna njia mbadala ya kusafirishwa kutokana na magari kushindwa kabisa kupita kwenye barabara hiyo.

## Walia konokono kula maharagwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa maharagwe Kata ya Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamedai imeibuka aina ya konokono ambao wanakula maharagwe na kuwasababishia hasara.

Wanadai kuwa wanalazimika kufanya kazi ya kuokota na kuwaua konokono hao kila siku mashambani, na kwamba bila kufanya hivyo mkulima hawezi kuambulia kitu kutokana na aina hiyo ya konokono kukata maharagwe kwenye shina ama kula matunda.

Joshua Soja, alisema konokono hao walianza kula maharagwe mwaka juzi, lakini mwaka huu wameleta madhara zaidi kutokana na kuharibu mashamba makubwa.

Alisema hawajawahi kuona konokono wakiharibu mazao, lakini miaka hii miwili wameshuhudia sehemu kubwa ya mazao yao yakiliwa hasa maharagwe, alizeti na kahawa.

"Tumejaribu kutumia dawa mbalimbali, lakini tumeshindwa hawafi, njia pekee tunayofaulu ni kuwaokota shambani na kuwaua ama kuwatupa mbali kazi ambayo inatugharimu muda mrefu sana," alisema Soja.

Josephine Jengela, ambaye anakaa Mbalizi alisema alilima ekari moja ya maharage katika Kijiji cha Itimba, lakini kutokana na kwamba alikuwa haendi mara kwa mara alikuta zaidi ya nusu ya shamba hilo maharage hayapo.

Alisema awali hakugundua kinachokata lakini alipowauliza wenyeji aliambiwa kuwa ni konokono na ndipo akaanza juhudi za kuokoa kidogo yaliyokuwa yamebaki.

"Niliamua kuajiri watu kwa ajili ya kuokota wadudu hawa maana ni wengi mno na wanzaliana haraka, ukiokota leo unakuta wapo hata wadogo wengi ambao ndani ya wiki moja wanakuwa tayari wakubwa na wanaanza kula maharagwe tena," alisema Josephine.

# RC ataka takwimu za VVU kugawanywa Mbeya, Songwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema mkoa huo unaonekana kuwa na takwimu kubwa za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU), kwa sababu hazikugawanywa wakati wa kuugawa mkoa huo na kuanzisha Mkoa wa Songwe.

Chalamila aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Kifua, Kikuu na Dawa za Kulevya iliyotembelea maeneo mbalimbali ya mkoa huo yanayotumika kukabiliana na maambukizi ya VVU.

Alisema takwimu hizo zilitakiwa zigawanywe kama walivyogawana mali, madeni na rasilimali zingine, na kwamba ingefanyika, kuna uwezekano takwimu zilizopo sasa hivi zingekuwa zimepungua na kufanya mkoa huo kutokuwa miongoni mwa yenye viwango vikubwa vya maambukizi.

Alisema kabla ya mwaka 2016, takwimu zozote za Mkoa wa Mbeya zilikuwa zinasoma mpaka katika Mkoa wa Songwe ambao ni miongoni mwa mikoa inayopakana na mataifa mengine ya Ukanda wa SADC, lakini kuna uwezekano kwamba wataalamu walisahau kugawa takwimu hizo baada ya kugawa mkoa.

"Kuna uwezekano kwamba hizi takwimu zinazosoma kwamba tuna asilimia 9.3 zingeshuka mpaka kwenye asilimia sita ili kuonyesha kwamba zingine zilikuwa za Mkoa wa Songwe, na pengine tusingekuwa miongoni mwa mikoa yenye viwango vya juu vya maambukizi," alisema Chalamila.

Alisema kabla Mkoa wa Mbeya haujagawanywa, ulikuwa na zaidi ya kilomita za Mraba 60,000, lakini baada ya kugawanywa ulibaki na kilomita za mraba 35,000 na Songwe una kilomita za mraba 35,000.

Mratibu wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), Mkoa wa Mbeya, Dk. Masili Lutaragula, alisema mkoa huo unaendelea na mikakati mbalimbali za kukabiliana na maambukizi mapya ya VVU.

Alisema moja kati ya mikakati wanayoendelea nayo ni kuhamasisha matumizi ya kondomu, ambapo alisema mpaka kufikia Disemba 2020, Mkoa huo ulisambaza kondomu zaidi ya milioni 3.14 kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kwenye ngazi ya jamii.

Vilevile, alisema wanaendelea kuhamasisha tohara ya hiyari kwa wanaume kutokana na tafiti za kitaalamu kubaini kuwa tohara inasaidia kupunguza maambukizi kwa asilimia 60 pamoja na kutoa huduma kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

"Vile vile tunaendelea kutoa elimu ya UKIMWI kwa jamii kuhusu mapambano dhidi ya janga hili, pia tunaendelea na kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na tunaendelea na huduma ya tiba na matunzo," alisema Dk. Lutaragula.

Mkurugenzi wa Shirika la Walter Read Tanzania, Dk. David Maganga, alisema kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, wameanzisha huduma ya tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na maambukizi.

Alisema vilevile, wameanzisha huduma ya kliniki kwa watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya ambayo inafanyika Jumamosi mbili kila mwezi kwa ajili ya kuchukua dawa, vipimo na ushauri.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya, Fatma Toufiq, aliupongeza Mkoa wa Mbeya kwa kuwa na mikakati mizuri ya kukabiliana na VVU, na kwamba ikitekelezwa vizuri, itasaidia kupunguza maambukizi.





# Rais Mwinyi ahimiza kilimo cha miwa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amevitaka vikosi vya ulinzi na usalama kuongeza nguvu katika shughuli za kilimo cha miwa, ili kukiwezesha kiwanda cha sukari Mahonda kuwa na malighafi ya kutosha.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja, alipokitembelea kiwanda hicho na kuangalia mchakato mzima wa uzalishaji wa sukari pamoja na kuzungumza na uongozi, wafanyakazi, wawakilishi wa wakulima wa nje pamoja na wawakilishi wa Vikosi vya Serikali ya Zanzibar.

Alivitaka vikosi vya ulinzi na usalama, ikiwamo Jeshi la Magereza, Jeshi la kujenga Uchumi (JKU) na Kikosi cha Valantia (KVZ) kupitia nguvu kazi waliyonayo, zana za kilimo na ardhi ya kutosha iliopo kuongeza juhudi na kuongeza uzalishaji wa miwa katika maeneo yao.

Alisema hali ya kilimo hicho ilivyo hivi sasa katika vikosi hivyo haiendani na uwezo halisi wa vikosi, hivyo akawataka kuongeza uzalishaji kwa kigezo kuwa kutawaongezea kiwango cha mapato.

Alieleza kuwa Serikali itazipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazokikabili kiwanda hicho, huku akiutaka uongozi wa kiwanda kuyatatua matatizo ya wafanyakazi mapema iwezekanavyo.

Alisema pamoja na mambo mengine, Serikali itaangalia bei ya sukari, pamoja na upatikanaji wa ardhi bora kwa ajili ya kilimo cha miwa sambamba na kuitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuwawezesha wakulima wa kilimo cha miwa kutumia njia ya umwagiliaji ili kiwanda hicho kipate malighafi zaidi.

Alisema kilimo cha miwa kinaweza kuwa mkombozi wa maisha ya wakulima, hivyo ni vyema Serikali ikatafuta maeneo mazuri ili yaweze kutumika kwa kilimo hicho.

"Watu kama wataweka mkazo katika kilimo cha miwa wataweza kubadili maisha yao," alisema.

Aidha, akatoa wito kwa wakulima wakubwa kujitokeza kuunga mkono ukulima wa kilimo cha miwa, sambamba na wakulima wadogo kuwezeshwa kwani kinaweza kubadili maisha yao.

Akigusia juu ya madai mbalimbali ya wafanyakazi wa kiwanda hicho, Rais Dk. Mwinyi alisema hapendi kusikia changamoto za wafanyakazi, ikiwamo kutokuwapo kwa mikataba, mishahara duni pamoja na kuchangia vifaa vya kazi, hivyo akaagiza kupatiwa ufumbuzi.

Naye, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema Wizara hiyo imekuwa ikifanya vikao mbalimbali kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi changamoto tofauti zinazokikabili kiwanda hicho.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahamoud, alisema uongozi wa mkoa huo umeunda kamati maalum inayolenga kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zilizokikabili kiwanda na kuchochea kushusha kiwango cha uzalishaji wa sukari.

Mkurugenzi wa kiwanda cha Sukari Mahonda, Rahim Bhaloo, alisema ushirikiano baina ya wizara na mwekezaji ndio njia pekee itakayowezesha utatuzi wa matatizo mbalimbali inayokikabili kiwanda hicho.

Aliiomba Serikali kusaidia kuwahamasisha wakulima kulima miwa katika maeneo mbalimbali, ambako ardhi ni nzuri kwa ajili ya kilimo katika mabonde madogo.

Aidha, aliiomba Serikali kupitia wataalamu wa kilimo, kuhakikisha maeneo yanayotolewa kwa kilimo cha miwa kwa ajili ya kiwanda hicho yanakuwa yenye rutuba na kuwezesha zao hilo kustawi vyema.

Aidha, wafanyakazi wa kiwanda hicho walilalamika kukosa mikataba ya ajira, kiwango duni cha mishahara wanacholipwa na kutakiwa kununua vifaa vya kufanyia kazi.



Mwandishi wa habari mwandamizi, Mahfoudha Alley, akizungumza wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake yalioandaliwa na Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanaoingia Z'bar kupima corona kimtandao

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, Wazee na Watoto itaanzisha vipimo vya corona kwa wasafiri wanaoingia na kutoka Zanzibar kwa njia ya mtandao kuanzia Machi 9, mwaka huu.

Uamuzi huo umeandaliwa ili kukabiliana na vyeti feki na kuondoa usumbufu na msongamano wa wasafiri kwenye vituo vinavyoendesha zoezi hilo Mazizini na Lumumba kwa Unguja na kituo kimoja kilichopo Pemba.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema Wizara inajiandaa kuanzisha vituo vingine katika maeneo yenye hoteli nyingi ili kuongeza ufanisi. Dk. Shajak alisema gharama ya kipimo cha corona imeongezeka kufikia dola 80 kwa wasafiri wote kutokana na kuongezeka gharama ya kununulia mashine za kupimia maradhi hayo.

Hata hivyo, alisema wananchi wa Zanzibar hawana haja ya kulalamika kupanda bei kipimo cha corona kwa sababu sio suala la matibabu bali ni matakwa ya mashirika ya ndege kwa wasafiri kulazimisha wawe na vyeti vya maradhi hayo.

Alisema kutoa bure kipimo hicho, kama zinavyotolewa huduma zengine za afya, ama kupunguza bei ni kuwaongezea mzigo wa maisha wananchi wengine bila ya sababu za msingi.

**Wakati huo huo,** Wizara hiyo imetiliana saini mkataba wa ushirikiano wa miaka mitatu na Hospitali ya SIMS ya India.

Kupitia mkataba huo uliotiwa saini na Dk. Shajak na Meneja wa nchi za nje wa SIMS. Zanzibar itafaidika kwa kuwapeleka wagonjwa India watakaoshindwa kupata matibabu Hospitali ya Mnazimmoja na hospitali za Tanzania Bara.

Dk. Shajak alisema maeneo mengine yaliyomo ndani ya mkataba huo ni kupatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi madaktari wa Zanzibar nchini India na madaktari bingwa kutoka Hospitali ya SIMS kuandaa kambi za uchunguzi wa maradhi mbalimbali kwa gharama zao na Serikali kuhudumia matibabu.

# Ataka watoto wa kike kuandaliwa kuwa viongozi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MWANDISHI wa habari mkongwe Zanzibar, Mahfoudha Aley Hamid, amesema iko haja ya watoto wa kike kuandaliwa ili kujitambua na kuwa viongozi baadae.

Akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu ushirikishwaji wanawake katika uongozi, alisema hatua hiyo itamuwezesha kumjengea ujasiri na kujiamini kwa kutambua umuhimu wa kushiriki harakati hizo.

Aidha aliesema wanawake wanakumbana na changamoto nyingi za ubaguzi hasa wa kijinsia na umri na ndio maana ushiriki wao katika uongozi ni mdogo.

Aidha alisema katika kero kubwa duniani ambayo bado ni changamoto nzito, ni idadi ndogo ya uongozi kwa wanawake katika sekta zote na uwakilishi wao kwenye ngazi ya uongozi bado ni ndogo sana.

" Hadi leo wanawake wanakabiliwa na sheria kandamizi, taasisi ambazo hazikidhi haja katika kumkomboa mwanamke na kumwendeleza katika kufikia ngazi ya uongozi na tabia mbaya iliyozoweleka ambayo inamnyima mwanamke fursa na kumfanya asipate nafasi kamili ya kushiriki kikamilifu katika kazi za umma akiwa kama kiongozi," alisema.

Alieleza kuwa wanawake hata wakiwa wengi katika taasisi, iwapo uongozi wa juu wa nchi na taasisi husika umehodhiwa na wanaume, wanawake watabaki wasindikizaji.

"Tukiangalia historia kuna wanaume wengi wa umri mkubwa ambao wanashika nyadhifa za juu kuliko wanawake. Wanawake wanakuwa wanafuata mapendekezo ya wanaume, hivyo wanakuwa waathirika."

Naye Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema waandishi wana jukumu katika kuleta mabadiliko, hivyo waandike habari hadi jamii itakapobadilika na kumkubali mwanawake.

Aliyataja maeneo ambayo ni muhimu katika kuyafanyia kazi ni upatikanaji wa haki ya usawa wa kijinsia ikiwamo idadi sawa katika ngazi za uamuzi .

Mafunzo hayo ya siku mbili kwa waandishi wa habari yana lengo la kukuza ushirikishwaji wanawake katika uongozi yameandaliwa na TAMWA Zanzibar.

HABARI KITAIFA

# Zimamoto yatoa elimu kujikinga majanga ya moto

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Jeshi la Zimamoto Wilaya ya Mkuranga, Fransisco Chunji, amewataka wananchi wa wilaya hiyo kuchukua tahadhari ya matumizi ya simu wakati wa mvua zinazoambatana na radi.

Alitoa rai hiyo katika Shule za Msingi za Binga, Kitomondo na Shule ya Sekondari Kiparang'anda, akiwa katika utaratibu wa jeshi hilo wa kutoa elimu dhidi ya majanga katika taasisi mbalimbali na mikutano ya wananchi.

Chunji alisema ili kuepuka maafa yanayo sababishwa na radi, wanafunzi wanatakiwa kuwa mabalozi wa kufikisha elimu hiyo kwa wazazi na walezi wao kutotumia simu wakati wa mvua kubwa na kwa nyumba zinazotumia umeme kuhakikisha zinakuwa na kidhibiti radi.

Alisema ili kuepuka ajali za kuporomoka kwa majengo, miti mikubwa karibu na nyumba za makazi inatakiwa kukatwa au kupunguzwa matawi. Alitoa angalizo kwa wananchi kuepuka kujenga nyumba mabondeni, pia kutengeneza njia ya maji kuepusha majanga yanayoepukika.

Akitoa elimu ya kuepuka majanga shuleni, Chunji alisema kila shule inatakiwa kuhakikisha wanafunzi wana elimu dhidi ya majanga, vifaa vya kuzimia moto vinafungwa katika maeneo yote muhimu bwenini, ofisini na maeneo ya stoo na mabweni yote yanafungwa mifumo ya kung'amua moshi.

"Vifaa hivyo husaidia kupiga kelele wakati wa tukio la moto na hivyo kurahisisha uokoaji wa mali katika chumba husika, tunaendelea kuwaasa wamiliki wa shule kuhakikisha vyumba vya maabara haviwi na mitungi ya gesi ndani badala yake iwekwe nje ya jengo katika chemba maalumu," alisisitiza.

Alisema ni wajibu wa kila mmiliki wa shule katika Wilaya ya Mkuranga kutoa taarifa ofisi ya Jeshi la Zimamoto iwapo anataka kuanzisha shule ili elimu dhidi ya majanga ianze kutolewa kuanzia kwenye ramani ya jengo ujenzi unapoendelea hadi wanafunzi wanapokuwa wameanza masomo.



Mwendesha pikipiki akiwa amepakia magunia manne ya mkaa ambapo huchukuwa nafasi kubwa barabarani na husababisha foleni ya magari kutokana na mwendo wake mdogo na magari kushindwa kuwapita kutokana na urefu wa mzigo aliobeba eneo la Kimara Temboni barabara ya Dar es Salaam -Morogoro juzi. **PICHA: SALOME KITOMARI**

## Wanawake kupewa nafasi Benki Standard Chartered

**Na Enock Charles**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake duniani leo, Benki ya Standard Chartered imeweka mpango mkakati wa kuwajumuisha wanawake katika uongozi wa juu wa benki hiyo ili kuhamasisha usawa wa kijinsia katika benki hiyo .

Akizungumzia matokeo ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) kuhusu usawa wa kijinsia katika benki hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, alielezea kufurahishwa na matokeo ya awali ya shirika hilo yaliyoonyesha benki hiyo ina utamaduni unaounga mkono usawa wa kijinsia .

"Nimefurahi kuona matokeo ya awali yaliyowasilishwa na IFC juu ya uchunguzi wa kijinsia ambao wamefanya kwenye Benki, Matokeo haya ya awali yanaonesha maendeleo makubwa ambayo tumefanya juu ya dhumuni letu pamoja na ajenda ya ujumuishaji." alisema Rughani.

## Wajasiriamali wadogo wanolewa biashara

**Na Zuwena Shame**

TAASISI ya Tanzania Data Lab (dLab) imetoa mafunzo ya taarifa na biashara kwa wajasirimali wadogo zaidi ya 45 kutoka Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Taasisi hiyo imetoa mafunzo kwa wajasirimali wa kike zaidi ya 150 kutoka Shinyanga, Kagera, Mbeya na Dar es Salaam kati ya Januari na Machi 2021.

Mafunzo hayo ya wiki moja lengo lake ni kuwawezesha wajasiriamali wenye biashara ndogo kuwa na uelewa wa kukuza biashara zao kwa kutumia taarifa na kukuza mitaji na hatimae kukua kiuchumi.

Mwanzilishi Mwenza wa Tanzania Data Lab na mkurugenzi wa sayansi ya data, utafiti na mafunzo , Mahadia Tunga, alisema taasisi hiyo imekuwa ikiendesha mafunzo hayo kila mwaka kwa wanawake waliopo maofisini ila kwa mwaka huu imekuwa tofauti kwani nguvu zaidi zimelekezwa kwa wajasiriamali wadogo wanawake.

Tunga alisema baada ya mafunzo hayo wajasiriamali hao wanawake wataweza kufanya baishara zao kwa kutumia taarifa kwa kujiamini na kufanya uamuzi wa biashara zao kikamilifu.

## Wazoa zawadi za mil. 200/- NMB MastaBata

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI 448 wa kampeni ya NMB MastaBata Sio Kikawaida wamekamilisha miezi mitatu ya droo hiyo wiki hii baada ya kujinyakulia zawadi mbalimbali za vifaa vya nyumbani, fedha taslimu, simu za mkononi na safari za kitalii ambapo thamani ya zawadi zote ni Sh. milioni 200.

Droo hiyo imehitimishwa katika fainali iliyofanyika Machi 4, 2021 makao makuu ya Benki ya NMB jijini Dar es Salaam kwa kupatikana washindi 12 ambao wawili kati yao walichagua zawadi ya safari ya kitalii itakayojumuisha watu wawili kwa siku nne, safari hizo ni Serengeti, Ngorongoro na Visiwa vya Zanzibar.

Waliobaki walichagua vifaa vya nyumbani ambavyo vilikuwa ni Runinga kubwa (Smart TV) yenye king'amuzi cha Dstv kilicholipiwa kwa miezi mitatu, Jokofu la milango miwili, simu ya mkononi aina ya Samsung Galaxy Note 20, Microwave, Mashine ya kuchuja maji (Water Dispenser) na computer mpakato (Laptop) iliyounganishwa na Printer.

Washindi hao ni Mohamed Said Ali aliyechagua vifaa vya nyumbani, Miriam Aidan Mongii (vifaa), Ally Abubakary Ally (vifaa), Indra Pratap Narain Pathak alichagua safari ya kitalii pamoja na Abshir Farah Gure pia alichagua safari.

Washindi waliobakia wote walichagua vifaa vya nyumbani ambao ni Mango Mechris Christopher, Mohamed Hisham Mohamed Nouman, Job Lay Naman, Clara Cynthia Mwinchumu, Alice W. Mariki, Harid Valentino Gange na Christabel Ilona Hiza.

Akizungumza katika hafla ya fainali hiyo jijini Dar es Salaam wiki hii, Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha, Benedicto Baragomwa, alisema kwenye shindano hilo katika fainali iliyohusisha washindi 12, kila zawadi ilikuwa na thamani ya Sh. milioni 8 hivyo jumla ya Sh. milioni 96 zilichukuliwa katika fainali.

"Ukiangalia zawadi za mwisho zinahusisha vifaa vya nyumbani na mbuga za wanyama ikiwamo Serengeti na Ngorongoro pamoja na Visiwa vya Zanzibar, maana yake tunataka kuimarisha utalii wa ndani. Vilevile msingi wa shindano hili ni kutaka wateja wetu wapunguze matumizi ya fedha taslimu, ndiyo maana tulitaka kila anayetumia kadi kufanya miamala kuwa sehemu ya washindi," alisema Baragomwa.

Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Nchini (GBT), Elibariki Sengasenga, alisema anawapongeza NMB kwa ubunifu wao, lakini pia kwa kipindi chote cha miezi mitatu walipokuwa wakiendesha kampeni hiyo walifuata taratibu zote za bodi hiyo.

HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis aongoza misa Iraq

**Baghdad,** IRAQ

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, ameadhimisha Ibada ya Misa katika Kanisa Katoliki la Walkadea la Mtakatifu Joseph, mjini Baghdad, jana.

Aliwasili kwenye mji wa Mosul na kufanya ibada katika moja ya makanisa yaliyoharibiwa na wapiganaji wa IS na kisha kufanya ibada maalumu katika mji wa Irbil, watu zaidi ya 10,000 walihudhuria.

Papa Francis anakuwa kiongozi wa kwanza wa kanisa hilo, kuongoza Misa kwa kutumia liturjia ya Ibada ya Kanisa Katoliki la Mashariki.

Papa Francis (84), aliwaambia waumini kuwa si matajiri na wenye nguvu ambao wamebarikiwa, bali wale wanaowahurumia ndugu zao.

Mkuu wa Kanisa Katoliki la Walkadea, Kardinali Louis Raphaeli I Sako, aliita ziara ya Papa Francis, kama iliyopokelewa kwa furaha na kanisa lote.

Juzi, Papa Francis alishiriki katika mkutano wa kihistoria na kiongozi wa Waislamu wa madhehebu ya Shia, Ayatollah Ali al-Sistani, kwenye mji mtakatifu wa Najaf.

Pia alilizuru eneo linaloaminika kuwa sehemu ya kuzaliwa Abrahamu.

Jana, Papa Francis alizuru eneo la Mosul ambalo lilikuwa ngome kuu ya kundi linalojiita Dola la Kiislamu, IS.

Ziara hiyo ni ya kwanza kufanywa na Papa Francis nje ya Italia tangu kuripotiwa kwa mara ya kwanza kwa maambukizi ya virusi vya corona duniani, jana. **DW**

**Jana, Papa alizuru eneo la Mosul ambalo lilikuwa ngome kuu ya kundi a Dola la Kiislamu, IS.**




Papa Francis akiwa amezungukwa na makanisa yaliyoharibiwa, akihudhuria sala kwa waathiriwa wa vita eneo la Hosh al-Bieaa, Church Square, Mosul, uliokuwa mji mkuu wa kundi la IS, nchini Iraq, jana. **PICHA: AP**

## Maelfu wapinga sheria kilimo India

**New Delhi,** INDIA

WAKULIMA nchini India wameandam]ana na kufunga barabara kupinga sheria mpya za kilimo, zilizowekwa na serikali.

Maelfu ya wakulima nchini India, waliondamana kupinga sheria hiyo, walionekana katika barabara kuu za ndani na nje ya mji mkuu wa New Delhi, ikiwa ni siku ya 100 ya maandamano hayo.

Waandamanaji walishiriki maandamano hayo kwa matrekta yao na kutoa kaulimbiu za kupinga sheria mpya ya kilimo.

Serikali ya India ilitunga sheria tatu, Septemba mwaka jana, ambazo zilileta uhuru wa sekta ya kilimo, kuondoa bei ya wastani na msaada wa sera za ununuzi.

Wakulima walisema kuwa sheria mpya za kilimo zitapunguza mapato yao, ziwape nguvu zaidi wafanyabiashara wa kati na hatimaye kuwaacha bila ardhi.

Kama sehemu ya maandamano, mara kwa mara kumekuwa na makabiliano kati ya polisi na wakulima.

Awamu ya 11 ya mazungumzo kati ya serikali na wakulima haikuleta matokeo.

Pendekezo la serikali la kusimamisha sheria kwa miezi 18 pia lilikataliwa na wakulima. **TRT**

## Ajali yaua, yajeruhi

**Multan,** PAKISTAN

AJALI ya treni iliyotokea Kusini mwa Pakistan, jana, imesababisha kifo cha mtu mmoja na kujeruhi wengine 40.

Ajali hiyo (pichani) ilitokea kati ya vituo vya Rohri na Sangi, Kusini mwa Mkoa wa Sindh na kusababisha kusitishwa kwa muda kwa matumizi ya njia zote mbili, Ofisa wa Reli, Kamran Lashari, alisema.

Ajali za treni ni za kawaida kutokea nchini Pakistan huku serikali ikitoa kipaumbele kidogo katika kuboresha mfumo wa usafiri huo.

Lashari alisema ajali hiyo ilihusisha mabehewa 18 yaliyotoka Karachi kuelekea mji wa Mashariki wa Lahore huku sita yakitumbukia shimoni.

Muhammad Arshad alisema giza na uharibifu katika eneo hilo unakwamisha juhudi za uokoaji.

Alisema mwili wa mwanamke aliyekufa na abiria 40 waliojeruhiwa, walipelekwa hospitalini katika miji ya karibu.

Haikufahamika mara moja ni abiria wangapi walikuwa kwenye treni.

Waziri wa Reli, Azam Sawati, alikiambia kituo cha runinga kuwa, ajali hiyo inachunguzwa na serikali itatoa fidia ya kifedha kwa familia ya mwanamke aliyekufa pamoja na majeruhi wote. **ABC NEWS**



## Ebola yaua 13 Guinea, DRC

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

NCHI ya Guinea na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), zimeripoti visa 29 vya virusi vya Ebola na vifo 13 hadi sasa.

Taarifa hiyo ni kwa mujibu wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha Afrika (Africa CDC). Afrika CDC, wakala maalum wa huduma ya afya wa Jumuiya ya Afrika wenye wanachama 55, uliripoti kiwango cha vifo cha asilimia 45 katika nchi hizo mbili.

Hadi sasa, kituo hicho kimeripoti visa 11, vifo vinne na waliopona wawili, huku Guinea ikithibitisha visa 18, vifo tisa na kupona wawili pia.

Mlipuko mpya wa ugonjwa huo katika nchi hizo mbili za Kiafrika unatuma salamu barani Afrika wakati bara likikabiliwa na janga la COVID-19.

Mlipuko wa virusi vya Ebola, Afrika Magharibi mwaka 2014 hadi 2016 ulisababisha vifo vya watu zaidi ya 11,300, na visa zaidi ya 28,600 vikirekodiwa. **XINHUA**

# DE GEA SASA AWINDWA PSG




**MANCHESTER,** England

KIPA namba moja wa Manchester United, David De Gea, anatajwa kuwindwa na klabu ya Paris Saint-Germain ya nchini Ufaransa, kuchukua nafasi ya Keylor Navas.

Kwa mujibu wa gazeti la Sun, David de Gea amekuwa akilengwa zaidi katika uhamisho huo kuelekea Paris Saint-Germain.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania anawaniwa na kocha wa PSG, Mauricio Pochettino, kuchukua nafasi ya Navas, baada ya kukaa miaka 10 pale Old Trafford.

De Gea ameona nafasi yake ikiwa chini ya shinikizo kutoka kwa Dean Henderson, lakini mkongwe huyo hadi sasa ameendelea na kazi yake ya kuanza kikosi cha kwanza.

De Gea amekuwa akifanya makosa mengi ambayo yamekuwa yakiigharimu timu kwa misimu ya hivi karibuni na inaonekana wazi kuwa anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Licha ya kuongeza mkataba msimu uliopita, De Gea alionyesha wazi nia ya kutaka kuondoka kwa 'Mashetani Wekundu' hao, huku Klabu ya Real Madrid ya Hispania ikitajwa kumuwania.

# Aguero aipasua kichwa Juventus

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imengia kwenye mbio za kuwania kumsajili strika wa Manchester City, Sergio Kun Aguero, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Ripoti zinaeleza kwamba, Juventus wanawania kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Argentina, wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Aguero mkataba wake na Man City unafikia tamati mwishoni mwa msimu huu, na hakuna dalili za kuonyesha anaweza kuongezewa.


Kama hataongezewa mkataba ina maana kwamba, Aguero ataondoka pale kwenye dimba la Etihad akiwa mchezaji huru.

Ripoti za nchini Italia zinaeleza kwamba, Juventus inafikiria kumchukua mshambuliaji huyo ili kuimarisha safu yake ambayo inaongozwa na nyota wa kimataifa wa Ureno, Cristiano Ronaldo.

Miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, wanaamini Aguero atakuwa msaada mkubwa akiwa na upatina na Ronaldo.

Hata hivyo, Aguero pia amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kule Barcelona kwenda kucheza pamoja na rafiki yake Lionel Messi.

Msimu huu umekuwa mgumu kwake, hasa kutokana na kusumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara na wiki iliyopita alicheza kwa mara ya kwanza tangu Oktoba, mwaka jana.






# *Salah sasa mtegoni Madrid, Barcelona*

**LIVERPOOL,** England

STRAIKA wa Liverpool, Mohamed Salah, amehusishwa na mpango wa kutaka kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Kwa mujibu wa gazeti la Hispania la Marca, nyota huyu anajiandaa kuhamia Hispania, huku klabu za Barcelona na Real Madrid zikitajwa kumuwaniwa.

Mshambuliaji huyo alionekana kutokuwa na furaha baada ya kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Chelsea Alhamisi, na taarifa zinasema kocha Jurgen Klopp sasa anafanya jitihada kurejesha furaha yake kikosini hapo.

Salah alijiunga na Liverpool mwaka 2017 akitokea Roma kwa dau la pauni milioni 37.8, na hadi sasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, amecheka na nyavu mara 118 katika mechi 189 alizocheza tangu alipowasili klabuni hapo.

Alikuwa sehemu muhimu sana ya kikosi cha Liverpool katika kutwaa mataji ya Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya kuwa na mafanikio klabuni hapo, taarifa za kuhitaji kuondoka hapo zimekuwa zikichukua taswira kubwa zaidi.

Kwa mujibu wa ripoti za hivi karibuni, wakala wa staa huyo wa Misri tayari ameshapanga mikutano na klabu zote mbili, Barcelona na Real Madrid, kipindi ambacho zote zitakuwa kwenye mawindo ya kuwania saini yake.

HABARI MICHEZO

# Juventus kuibomoa Chelsea

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus ya Ligi Kuu Italia Serie A, ipo kwenye hesabu za kuiwania saini ya kiungo wa Chelsea, Jorginho ili awe ndani ya kikosi hicho msimu ujao.

Nyota huyo ambaye yupo mikononi mwa kocha Thomas Tuchel ambaye ametua hapo kuchukua mikoba ya Frank Lampard aliyefukuzwa, anatajwa kuwa kwenye hesabu za Kocha Mkuu wa Juventus, Andrea Pirlo kwenye usajili wa msimu huu.

Licha ya Juventus kumhitaji Jorginho, utakuwa ni mpango wa pili ikiwa hesabu za chaguo lao la kwanza la kuipata saini ya Manuel Locatelli ambaye ni kiungo bora ndani ya kikosi cha Sassuolo na dau lake linatajwa kuwa pauni milioni 30.

Hata hivyo, ripoti zimeeleza kwamba Juve hawapo tayari kutoa zaidi ya pauni milioni 30, jambo ambalo limewafanya wafikirie mbadala wa kumpata kiungo mwingine.

Na Jorginho raia wa Italia mzaliwa wa Brazil, anaonekana kwamba, ndiye anayefaa zaidi kwa kikosi hicho.

Kwa mujibu wa Calciomercatio, Juverntus walianza kumuweka Jorginho kwenye rada tangu zama za Maurizo Sarri akiwa ni kocha mkuu, jambo ambalo linawafanya wawe na uhakika wa kile wanachokifanya.





# IBRAHIMOVIC KUREJESHWA TIMU YA TAIFA SWEDEN

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic anatarajia kurejeshwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Sweden mwezi huu, kwa mujibu wa ripoti mbalimbali za soka.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 39, aliamua kuachana na soka la kimataifa mwaka 2016, lakini sasa yupo tayari kurudi kuichezea tena timu hiyo.

Ibrahimovic anatarajiwa kuitwa tena kwenye timu ya Sweden kwenye likizo ijayo ya kimataifa, wakati kikosi hicho kikijiandaa kuumana na Kosovo, Georgia na Estonia.

Nyota huyo amekuwa na kiwango bora zaidi cha kuvutia akicheza pale AC Milan, hivyo inaonekana anaweza kuwa na mchango mkubwa kwa timu ya taifa.

Awali iliripotiwa kwamba, Ibrahimovic alitembelewa mazoezini na kocha mkuu wa Sweden, baada ya kuona anazungumzia suala la kurejea dimbani kwenye timu ya taifa.

# Kroos kustaafia Madrid

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Real Madrid, Toni Kroos, amesema ana mpango wa kumalizia soka lake akiwa na miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Kroos amefurahia mafanikio mbalimbali makubwa tangu ajiunge na Madrid akitokea klabu ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich mwaka 2014.Ameshinda mataji ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu, LaLiga mara mbili na pia kutwaa mataji mengine 13 kwa kipindi alichocheza kwenye timu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amecheza mechi 309 kwa Real madrid katika mashindano yote na anakuwa raia wa kwanza wa Ujerumani aliyecheza mechi nyingi zaidi baada ya Uli Stielike.

Kroos ambaye amefanikiwa kufunga mabao 21 tangu atue katika klabu ya Madrid, aliiambia Madrid TV: "Ni kitu maalumu, unapoangalia Wajerumani ambao wamecheza hapa unagundua kuwa wana majina makubwa: Gunter Netzer, Bernd Schuster au Stielike.

"Kumpita Stielike ambaye ni gwiji katika klabu, inanifanya niwe na furaha sana, ni rekodi maalumu ninajivunia kufikia hatua hii.

"Kama nisemavyo siku zote, wazo langu ni kumalizia soka hapa na hicho ndiyo ninaenda kukifanya."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XHAKA SASA AWAANGUKIA MASHABIKI BAO ARSENAL

Nakunja mikono yao na naomba samahani kwa kosa lile, kwa sasa najiona kama nimewaweka...

**LONDON,** England

GRANIT Xhaka ameomba radhi kwa mashabiki wa Arsenal baada ya kosa lake kuizawadia Burnley bao la kusawazisha kwenye sare ya 1-1 juzi, Jumamosi kwenye Uwanja wa Turf Moor.

**'Washikabunduki' hao walianza kwa kuongoza kupitia kwa Pierre-Emerick Aubameyang aliyeunganisha pasi nzuri ya Willian.**

Xhaka alipewa pasi fupi kutoka kwa golikipa, Bernd Leno na wakati akijaribu kumpasia David Luiz, akajikuta akipiga mpira kuelekea langoni mwake na kumkuta straika, Chris Wood aliyefunga bao la kusawazisha.

Tukio hilo liliigharimu Arsenal na kushindwa kuondoka na pointi tatu kwenye mchezo huo. Baada ya mchezo huo, Xhaka akaomba radhi kwa mashabiki kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Nakunja mikono yao kuhusu bao lile na naomba samahani kwa kosa lile," aliandika Xhaka.

"Hiyo ndilo soka na kwa sasa najiona kama nimewaweka kwenye wakati mbaya mashabiki wote."

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alikataa kumshutumu Xhaka baada ya mchezo huo, akisisitiza, anataka wachezaji wake kuwa na utulivu, kwani makosa ni jambo la kawaida kwenye soka.

"Tunazungumza kuhusu mabao rahisi, hilo si jambo muhimu kwa sasa, makosa ni sehemu ya soka," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Wiki chache zilizopita, tumefanya hivyo. Tunatakiwa kuimarika ili kuendelea kupata matokeo, na mwisho wa siku tunatakiwa kufanya uamuzi nje ya uwanja na ndani ya uwanjani.

"Na si jambo rahisi kucheza nje ya nyumbani, lakini kama kuna mtu anafanya makosa kwa sababu wanacheza kwa staili ambayo tunataka kucheza."

Sare hiyo imeifanya Arsenal kubaki nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi tisa nyuma nje ya nne bora.

## ZISIKUPITE

### BAYERN KUMNUNUA HAALAND

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick, amesema kuna "uwezekano mkubwa" wa klabu hiyo kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, 20. ***(Mail)***

### LIVER YAJITOSA KWA MBAPPE

LIVERPOOL imeingia kwenye mbio moja na Real Madrid katika kuwania saini ya mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe, 22, ikiwa mshambuliaji wao, Mohamed Salah, 28, ataondoka klabuni hapo. ***(AS)***

### PSG WAMTAKA DE GEA

KLABU ya Paris St-Germain wanamnyatia golikipa wa Manchester United na Hispania, David de Gea, 30, na huenda wakamnunua msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### BARCA KUMKOSA TRAORE

BARCELONA inakabiliwa na changamoto za kifedha huenda ikashindwa kumnunua mshambuliaji wa Wolves na Hispania, Adama Traore, 25. ***(Mundo Deportivo)***

### SASA AGOMBEWA ULAYA

WEST Ham wamejiunga na RB Leipzig na Roma katika mbio za kumsaka mshambuliaji wa Austria, Sasa Kalajdzic, 23, ambaye Stuttgart wako tayari kumuuza kwa karibu pauni milioni 15. ***(Mail)***

### WATZKE AFUNGUKA DORTMUND

MTENDAJI Mkuu wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke, amesema hatarajii kupokea dau kubwa msimu huu kwa ajili ya winga wao, Erling Haaland, 20 au nyota wa England, Jadon Sancho. ***(Goal)***

### MAN CITY WAMTAKA RABIOT

MANCHESTER City wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Juventus, Adrien Rabiot, 25, lakini Everton pia wanamnyatia nyota huyo wa Ufaransa. ***(Tuttosport)***

### POGBA BADO HEKIELEWEKI

KLABU ya Manchester United ipo gizani kuhusu hatma ya kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, kwa sababu hakuna majadiliano yoyote yanayoendelea kati ya klabu hiyo na wakala wake, Mino Raiola. Mkataba wa Pogba unakamilika mwisho wa msimu huu. ***(Star)***

### RAPHINA AWANIWA UNITED

MANCHESTER United wamewasilisha dau la kutaka kumnunua winga wa Leeds United, Mbrazil Raphinha, 24, wakati dirisha la uhamisho wa wachezaji litakapofunguliwa. (UOL Esporte)

### SILVA BADO AWINDWA

MANCHESTER United wanajiandaa kushindana na Atletico Madrid katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Andre Silva mwenye miaka 25. (Todofichajes)

HABARI MICHEZO

# Mashabiki wavutiwa na Ligi ya Wanawake

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza mashabiki wa soka nchini Tanzania walishuhudia laivu mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam Ijumaa iliyopita kati ya klabu mbili hasimu nchini Simba na Yanga, ikiacha gumzo na baadhi ya wachezaji kuwavutia wengi. wakitaka pia baadhi ya michezo iendelee kuonyeshwa.

Mara baada ya kumalizika mechi hiyo, mitaani na kwenye mitandao ya kijamii imekuwa ikizungumziwa sana tofauti na ilivyokuwa huko nyuma, huku wacheza Mwanahamisi Omari, Mawete Musolo, Joel Bukuru, Opa Clement na Janeth Shija kwa upande wa Simba wakiwa gumzo kutokana na uwezo mkubwa walioonyesha, wakati Aisha Masaka na Husna Zuberi kwa upande wa Yanga nao wakiwa midomoni mwa mshabiki.

"Nimefurahi, unajua zinapocheza timu hizi pinzani ni lazima mchezaji ucheze mara mbili ya vile unavyocheza siku zote, ndiyo maana umeona tumejituma zaidi, pia wenzetu walikuwa wanaongoza ligi kwa muda mrefu, ushindi wa mechi hii ulikuwa unaturudisha kileleni," alisema nahodha wa Simba, Mwanahamisi ambaye ni maarufu kwa jina la Gaucho.

Gaucho pia amesifu jinsi Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Wadhamini wa Ligi Kuu, kuamua kuionyesha mechi hiyo na kufanya watu wengi waone vitu ambavyo wanawake wanaweza kufanya kama wanaume.

Husna alisema kuwa wamepoteza mechi kutokana na makosa waliyoyafanya na watayarekebisha kwani ligi bado haijaisha.

Mashabiki tayari wameshaanza kuwapa majina wachezaji, kwani Mawete, kiungo kutoka DR Congo akipachikwa jina la Chama na mashabiki wa Simba kutokana na uwezo wake mkubwa wa kupiga chenga za maudhi, pasi za uhakika na utulivu mkubwa.

# MSUVA AWIKA TENA, AIPAISHA WAYDAD MABINGWA AFRIKA

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva, ameendelea kung'ara katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya juzi, Jumamosi kuipasha kileleni timu yake ya Wydad Casablanca kwa kuifungia bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Horoya FC ya Guinea.

**Bao hilo linamfanya Msuva sasa kuifungia timu hiyo mara mbili mfululizo kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), baada ya mechi iliyopita kufunga moja wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Kaizer Chiefs FC ya Afrika Kusini.**

Katika mchezo wa juzi, uliopigwa Uwanja wa Mohamed V jijini Casablanca, Morocco, Msuva, nyota wa zamani wa klabu ya Yanga alifunga bao hilo dakika ya 90 akimalizia kazi nzuri iliyofanywa na Ayoub El Kaabi, aliyefunga bao la kwanza dakika ya 19 kwa pasi ya mshambuliaji mwenzake Mmorocco, Walid El Karti.

Kwa ushindi huo, Wydad sasa inafikisha pointi tisa na kuendelea kuongoza Kundi C, ikifuatiwa na Horoya yenye pointi nne sawa na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini wakati Petro Atletico ya Angola inashika mkia ikiwa haina pointi baada ya wote kucheza mechi tatu.

Lakini pia Wydad inaungana na Mamelods Sundowns ya Afrika Kusini kutoka Kundi B, kuwa timu pekee katika hatua ya makundi ya michuano hiyo msimu huu ambazo hazijapoteza mechi hata moja hadi mzunguko huu wa kwanza unamalizika.

Timu zingine zilizofanya vizuri hadi sasa mbali na Wydad na Memelodi, ni Simba ya Tanzania kutoka Kundi A na Esperance ya Tunisia kutoka Kundi D, ambazo zimemaliza mzunguko wa kwanza zikiwa zikiwa kileleni mwa makundi yao kwa kufikisha pointi saba.

Simba ipo kundi moja na Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo ambazo zimemaliza mzunguko wa kwanza zikiwa na pointi nne wakati timu nyingine ya kundi hilo, Al-Merrikh ya Sudan ikiburuza mkia kwa pointi moja.

Kwa upande wa kundi la Esperance inafutiwa na MC Alger ya Algeria yenye pointi tanio El Zamalek ya Misri pointi mbili huku Teungueth FC ya Senegal ikiburuza mkia na pointi moja.

## USHOROBA MARATHON...




Waziri wa TAMISEMI, Suleiman Jafo (kushoto), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Abdallah Ulega (wa pili kulia), Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald (kulia) na Mhifadhi Mazingira kutoka WWF, Dk. Severin Kalonga, wakiwa kwenye picha ya pamoja na washindi wa jumla wa mbio za Kisarawe Ushoroba Marathon Km 21, Omary Maulidi (katikati), Rebecca Machege (kushoto) na Grace Charles, zilizodhaminiwa na Vodacom na kufanyika wilayani wilayani Kisarawe, Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Namungo matumaini kibao wakiwafuata Wamorocco*

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha timu ya Namungo kimewasili jijini Dar es Salaam jana kikitokea mkoani Kagera moja kwa moja na kuanza safari ya kuelekea nchini Morocco tayari kwa mechi yao ya hatua ya makundi dhidi ya Raja Casablanca itakayopigwa keshokutwa, Jumatano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, alisema walitarajia timu yao iondoke jana saa nne.

"Tunatarajia kuondoka leo usiku au kesho (leo) asubuhi lengo ni kwenda kufanya vizuri na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania, alisema Hassan.

Alisema baada ya kupata pointi sita kwenye michezo yao miwili ya ugenini waliyoicheza, hayo ni maandalizi tosha kuelekea kwenye mchezo huo wa kimataifa.

Mwenyekiti huyo alisema kuna watu waliwatanguliza mapema nchini Morocco kwa ajili ya kwenda kuandaa mazingira ya timu itakaposhukia kabla hawajafika ikiwa ni pamoja na kukwepa hujuma.

Alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri na kwamba wataondoka na wachezaji 29, viongozi watatu na benchi la watatu.

Katika mechi hiyo ya juzi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Namungo ilishinda 1-0, shukrani kwa mfungaji Sixtus Sabilo dakika ya 68, ushindi ambao Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morroco, alisema utawaongezea hali ya kujiamini kuelekea kwenye mechi hiyo ya kimataifa .

"Ilikuwa ni kazi kubwa ndani ya uwanja ila mwisho wa siku tumepata ushindi, hiyo ni furaha kwetu kwa kuwa imetuongezea hali ya kujiamini kuelekea kwenye mechi zetu za kimataifa.

"Tulikuwa tunahitaji pointi tatu nasi tumepata hivyo pongezi kwa wachezaji pamoja na sapoti kutoka kwa mashabiki ambao wamekuwa nasi bega kwa bega," alisema Morocco.

# Michezo

Jumatatu Machi 8, 2021

Nipashe



Xhaka awaangukia mashabiki bao Arsenal UKURASA 22

WANGU HUU...




Kipa wa Arsenal, Bernd Leno, akiwahi na kudaka shuti lililoelekezwa langoni mwao kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Burnley iliyopigwa Uwanja wa Turf Moor juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yabebeshwa sare Polisi

## ●●● Yazidi kuiachia njia Simba Fiston akifungua rasmi akaunti ya mabao Ligi Kuu huku...

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa zamani wa Yanga Paul Buswita, jana alikatisha furaha za mashabiki wa timu hiyo alipoisawazishia timu yake ya sasa Polisi Tanzania dakika moja kabla ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika na kuifanya mechi hiyo iishe kwa sare ya bao 1-1.

**Tayari baadhi ya mashabiki wa Yanga walikuwa wakifurahi na wengine kutoka kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha wakidhani wataondoka na ushindi wa bao 1-0, lakini Buswita, aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Kassim Shaaban aliuweka mpira wavuni na kuilazimisha Yanga kukubali sare na 'Walinda Usalama' hao wa nchi, Polisi.**

Ulikuwa ni mpira wa faulo iliyopigwa na Deusdedity Cosmas ukatua kwenye kichwa cha mfungaji akaujaza wavuni, akimuacha kipa Metacha Mnata akiruka baada ya mpira kujaa wavuni.

Ni bao lililoingia dakika moja tu baada ya beki wa zamani wa Yanga, Kelvin Yondani ambaye naye anaichezea Polisi Tanzania kwa sasa, kulimwa kadi nyekundu kutokana na kumchezea vibaya mfungaji wa bao la kwanza la Yanga, Fiston Abdulrazack.

Awali Yondani alionyeshwa kadi ya njano kwa kumchezea rafu mchezaji huyo raia wa Burundi.

Kushindwa kuibuka na ushindi kwa Yanga kulitokana zaidi na kuamua kujilinda kwa muda mrefu wa kipindi cha pili baada ya kupata bao dakika za mwisho za kipindi cha kwanza.

Awali Yanga iliandika bao la kwanza dakika ya 41, Fiston alipofunga kwa kisigino, akiunganisha krosi ya Tuisila Kisinda kutoka upande wa kulia.

Ni bao la kwanza kwa Fiston kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara tangu asajiliwe kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Niyonzima aliikosesha Yanga bao, alipopata krosi kutoka kwa Kisinda, mabeki wa Polisi Tanzania wakidhani mpira umetoka, lakini alijiandaa sana, kiasi cha mabeki kurejea golini na shuti lililopigwa kuwababatiza, likarejea uwanjani.

Shambulizi la hatari zaidi ambalo Polisi Tanzania ilifanya kipindi cha kwanza lilikuwa ni la dakika ya 29, straika Kassim Shaaban alimpomzidi nguvu Said Makapu na kupiga shuti kali akiwa ndani ya eneo la hatari na mpira kugonga mwamba wa juu na kurejea uwajani.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, lakini yaliinufaisha zaidi Polisi Tanzania kutokana na mchezaji wake aliyetoka benchini kufunga bao.

Kwa matokeo hayo, Yanga bado inaendelea kuwa kileleni ikiwa imefikisha pointi 50, tano mbele ya Mabingwa Watetezi, Simba, lakini vinara hao wakiwa mechi nne mbele. Simba imecheza mechi 19, Yanga ikicheza mechi 23. Pia kwa sare hiyo Polisi Tanzania bado ipo kwenye nafasi ile ile ya nane ikiwa na pointi 29 kwa mechi 22 ilizocheza.

Hivyo kama Simba ikishinda viporo vyake vinne, itaizidi Yanga kwa pointi saba.

# Gomes afunguka Morrison kuachwa

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, Mfaransa Didier Gomes, ameweka wazi uvumi unaomhusisha na kugombana na winga wa timu hiyo, Mghana Bernard Morrison, kwa kueleza hakuna kitu kama hicho na wana uhusiano mzuri.

Gazeti moja la Kiingereza lilichapisha taarifa ya kuwapo kwa ugomvi kwa wawili hao, na kisha taarifa hiyo kutafsiriwa kwa kiswahili na mtangazaji mmoja wa redio kisha kuiposti katika mtandao wake wa kijamii wa Instagram, jambo ambalo lilizua maneno mengi.

Jana baada ya Simba kuwasili ikitokea Sudan ilipolazimisha sare tasa dhidi ya Al-Merrikh kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Gomes na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez wakakanusha vikali taarifa hizo wakidai ni uvumi tu.

Gomes alipoulizwa na mwandishi wetu kuhusu sakata hilo, alisema: "Hakuna ugomvi wowote kati yangu na Morrison, niamini mimi, ninaweza kusema tuna uhusiano mzuri tunazungumza pamoja na nimemweleza malengo yangu, unajua kikosi ni familia tunahitaji kufanya kazi kama familia.

"Kila kitu ni kizuri na kama nilivyosema tukiwa Mbeya, ninajua atatusaidia kutimiza malengo yetu, suala la kumuacha kikosini ni la kifamilia, unajua kikosi ni familia tunahitaji kufanya kazi kifamilia."

Kwa upande wa Barbara, alisema Suala la Morrison ni uongo na kuachwa kwake ni suala la kiufundi tu.

"Hiyo inanikumbusha wakati ule ilipotengenezwa stori kuhusu Kagere (Meddie) kuwa amepigana na kocha (Sven Vandenbroeck), Morrison ni mchezaji mwenye nidhamu kubwa, hana tatizo na hakuna ugomvi wowote, unajua stori hizi si nzuri kwa sababu zinamfanya mchezaji ajisikie vibaya," alisema Barbara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >